# Nipashe

Jumatano Juni 17, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580260

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710




## Wanafunzi 100 wapata mimba kipindi cha corona

UKURASA 4



Mwamko mpya haki za weusi Floyd alipouawa

Ukurasa 13

siasa

JUMATANO JUNI 17, 2020

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Ni kiama mamluki kura za maoni CCM...

Ukurasa 12

Mifumo, miongozo, taratibu vitanzi vinavyokwamisha kufikiwa 50/50

Na Mary Geofrey

Profesa Ruth Meena, mwana zuoni wa sayansi ya siasa akitoa nasaha zake. PICHA MTANDAO.

SHERIA ZILIZOPITIWA

MFUMO WA UCHAGUZI

HAKI KUPIGA KURA

HAKI KUTEULIWA

INAENDELEA UK.12

UKURASA 11

# JPM: Maisha yaendelee

- Aagiza shule zote kufunguliwa Juni 29, harusi pia, aonya kampeni za matusi, ampongeza Shein kutua mzigo...

Endelea *Uk.* 2,3



Rais John Magufuli akihutubia Bunge, kabla ya kulivunja jijini Dodoma jana. Kulia ni Spika wa Bunge, Job Ndugai na kushoto ni Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

## MBOWE AJITOSA URAIS, AFUNGUKA

UKURASA 5

## Wamiliki shule waja na maagizo

UKURASA 5




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store


## BAA LA CORONA



Kwa maduka yanayouza bidhaa za chakula wafanyakazi wanatakiwa kuzingatia usafi wa sehemu zinazohifadhiwa bidhaa hizo ili kujikinga na virusi vya corona. WHO

- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

**MICHEZO** YANGA YATAMBA KUIADHIBU JKT UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Magufuli: Maisha yaendelee

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

RAIS John Magufuli ametangaza kufunguliwa kwa shule zote ifikapo Juni 29, mwaka huu, kutokana na kupungua kwa maambukizi ya virusi vya corona nchini.

Katika hotuba yake ya kufunga Bunge la 11 bungeni jijini hapa jana, Rais Magufuli alisema maambukizi ya virusi hivyo vinavyosababisha homa kali ya mapafu, yamepungua kwa kiwango kikubwa nchini.

Sambamba na hilo, Rais Magufuli pia alitangaza kuruhusu kufanyika kwa shughuli za kijamii zilizokuwa zimezuiwa kutokana na mlipuko wa virusi hivyo, ikiwamo harusi.

Licha ya tamko lake hilo, Rais aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi ya virusi hivyo vinavyoitesa dunia kwa sasa.

"Kutokana na hali ya ugonjwa wa corona kuendelea vizuri, na kwa kweli imepungua sana. Ninapenda fursa hii kutangaza kwamba kuanzia tarehe 29, ninafikiri itakuwa Jumatatu, mwezi huu wa Juni, shule zote zifunguliwe, zilizokuwa zimebaki.

"Lakini shughuli zingine, ambazo tulizizuia; watu kufunga ndoa, tumewacheleweshа watu kuoana wakati huu, nazo ziendelee. Maisha ni lazima yarudi kama ilivyokuwa zamani.

"Hata hivyo, ninaendelea kuwasihi Watanzania, kuendelea kuchukua tahadhari na pia kuzingatia ushauri unaotolewa na wataalamu wetu wa afya," Rais aliagiza.

Virusi vya corona viligundulika mwishoni mwa mwaka jana mjini Wuhan, China. Mpaka jana saa 8:30 mchana, kulikuwa na watu 8,141,521 walioambukizwa virusi hivyo katika mataifa na maeneo ya utawala duniani, vifo vikiwa 439,713.

Tanzania iliripoti kisa cha kwanza cha corona Machi 16, mwaka huu. Siku moja baadaye, serikali kupitia kwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ilitangaza kuzifunga shule na vyuo vyote, kwa lengo la kudhibiti kasi ya maambukizi.

Juni mosi, mwaka huu, serikali kupitia kwa Rais Magufuli, ilitangaza kufungua vyuo na jana Rais alitangaza kufungua shule baada ya juzi Waziri Mkuu (Majaliwa) kuliarifu Bunge kuwa nchi ina wagonjwa 66 tu wa corona.

Baa hilo limeathiri sekta mbalimbali, ikiwamo ya utalii inayochangia asilimia 25 ya fedha zote za kigeni nchini pamoja na ya kilimo kutokana na nchi kushindwa kuuza baadhi ya mazao yake ya kibiashara, hasa chai baada ya mnada wa Nairobi, unaotegemea na Tanzania, kufungwa.

Kufunguliwa kwa shule kutakuwa faraja kwa walimu takriban 90,000 wa shule binafsi waliolazimika kuishi bila mishahara kwa miezi minne baada ya shule kufungwa kutokana na janga la corona.



Marais wastaafu wakifuatilia hotuba ya Rais John Magufuli (hayupo kwenye picha), wakati akilivunja Bunge la 11 jijini Dodoma jana. Kulia ni Rais wa Awamu wa Pili, Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, Rais wa Awamu ya Nne Jakaya Kikwete na Makamu wa Rais wa Awamu ya nne, Dk. Ghalib Mohamed Bilal. **PICHA: OFISI YA BUNGE**.

# Rais aonya kampeni za matusi, ampongeza Shein

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS John Magufuli amevitaka vyama vya siasa na wanasiasa kujiepusha na kampeni za matusi na kejeli katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Angalizo hilo aliitoa jana bungeni alipokuwa akivunja Bunge la 11 lililohitimisha shughuli zake juzi chini ya Spika wa Bunge, Job Ndugai.

Alisema uchaguzi ni sehemu muhimu ya kukuza demokrasia na serikali imejipanga kuhakikisha uchaguzi wa mwaka huu unafanyika kama ilivyo zingine zilizopita unakuwa uhuru na haki.

"Tutasimamia uhuru na haki kwa vyama vyote na hii ndio demokrasia ya kweli, kwa sababu hiyo navisihi vyama na wanasiasa kujiandaa vizuri kushiriki katika uchaguzi huu, navihimiza pia vyama vitoe fursa ya kutosha kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu," alisema.

Aliwasihi wagombea kujiepusha na matusi na vurugu.

"Nchi hii ni yetu, hii Tanzania ni yetu sisi wote tuepuke sana shetani wa matusi, tumtangulize Mungu katika kampeni zetu, matusi na kejeli hayajengi, sisi sote ni wamoja, hivyo tubishane kwa hoja na kushindanisha ilani zetu," alisema.

Alisema kwa mtu yeyote atakayetaka kuleta vurugu anamtahadharisha kuwa serikali ipo macho na haijalala.

"Uchaguzi haumaanishi serikali imeenda kulala, itaendelea kuwapo kusimamia taratibu na sheria za nchi," alisema.

Aidha, alivishukuru vyama vya siasa vilivyotoa ushirikiano kwa serikali kwa miaka mitano iliyopita.

"Sisi sote ni wamoja na tunajenga Taifa moja, hivi ndivyo inatakiwa iwe," alisema.

Akizungumzia utendaji kazi wa mawaziri, Rais Magufuli alisema: "Watu hawa wamefanya kazi kubwa sana, wamenivumilia sana, wakati mwingine hawakuwa na uhakika na uwaziri wao, lakini wamechapa kazi sana.

**AMPONGEZA SHEIN**

Nampongeza pia Rais Ali Shein anayemaliza muda wake kwa mujibu wa Katiba amefanya kazi iliyotukuka nampongeza sana."

# ...Amwomba radhi mume wa waziri

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

RAIS John Magufuli ameendelea kumpongeza Waziri Ummy Mwalimu kwa utendaji mzuri, huku akimwomba radhi mume wa Waziri huyo wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kutokana na kumpigia simu mkewe usiku mnene wakati wa mlipuko wa corona.

Katika hotuba yake ya kufunga Bunge la 11 bungeni jijini hapa jana, Rais Magufuli alisema mlipuko wa virusi hivyo vinavyosababisha homa kali ya mapafu, ndiyo kikwazo kikubwa zaidi katika uongozi wake wa miaka mitano Ikulu.

Alisema kuwa katika mapambano dhidi ya corona nchini, 'alimtesa' kwa kiasi kikubwa Waziri Ummy kutokana na kumpigia simu mara kwa mara kwa lengo la kupata taarifa na kumpa maelekezo ya kufanyiwa kazi.

"Kuna mama shujaa Ummy Mwalimu, amefanya kazi kubwa katika kukabiliana na corona. Nilimtesa sana waziri huyu. Niombe radhi kwa mume wake, nilikuwa ninampigia simu hadi saa nane usiku," alisema.

WALIOKIMBIA BUNGE

Rais Magufuli pia alikosoa kitendo cha baadhi ya wabunge wa vyama vya upinzani nchini kuukimbia mkutano wa Bunge la Bajeti kutokana na tishio la corona.

Alikumbusha kile kilichoandikwa na Chinua Achebe kwenye kitabu chake cha 'Things Fall Apart' kwamba matatizo hayatatuliwi kwa kuyakimbia, akisisitiza kuwa kukimbia tatizo ni ishara ya uoga, udhaifu na kutokujiamini.

"Corona ndiyo kikwazo kikubwa zaidi tulichokumbana nacho. Ninalishukuru Bunge kwa kupitisha azimio la kunipongeza, lakini pongezi hizi ni kwa Watanzania wote na Bunge hili ambalo licha ya corona, liliamua kuendelea na vikao vyake.

"Wapo wachache waliwakimbia, sijui kama wamerejea. Kukimbia halikuwa jambo sahihi, matatizo hayakimbiwi. Kukimbia ni ishara ya udhaifu, ni ishara ya uoga, ni ishara ya kutokujiamini.

"Siku zote njia sahihi ya kutatua matatizo ni kukubali kukabiliana nayo. Sisi tulikubali kukabiliana na corona, huku tukichukua tahadhari ya maambukizi na kumtanguliza Mungu," alisema.

Aliongeza kuwa kwa kufanya hivyo, wameokoa ajira za Watanzania na nchi sasa ina uhakika wa usalama wa chakula, tofauti na mataifa mengi ambayo yalichukua uamuzi wa kufunga mipaka na kuwafungia ndani wananchi wake.

Rais Magufuli pia alimpongeza Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, kwa kumpa ushirikiano mkubwa katika miaka yote mitano ya uongozi wake Ikulu.

## HABARI KITAIFA

# Spika Ndugai awahakikishia wabunge mafao

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge Job Ndugai, amesema tayari miswada sita ikiwamo wa Sheria ya Fedha 2020 uliopitishwa na Bunge juzi katika mkutano wa 19 imesainiwa na Rais John Magufuli na kwamba tayari mafao ya wabunge yameanza kuingizwa.

Kauli hiyo aliitoa jana bungeni alipokuwa akitoa taarifa ya shughuli zilizofanywa na Bunge la 11 katika mkutano huo, wakati Rais Magufuli akivunja bunge hilo.

Alisema Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali namba 2 kwa mwaka 2020, Muswada wa Sheria ya Afya ya Mimea 2020, Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu 2020, Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 3 mwaka 2020.

Mingine ni Muswada wa Matumizi ya Fedha za Serikali Mwaka 2020 na Muswada wa Sheria ya Fedha 2020.

"Kwa utendaji kazi wa Rais wa namna ambayo isiyokuwa na ulinganifu tayari amesaini miswada yote sita ikiwa ni pamoja Sheria ya Fedha namba 8 ya mwaka 2020, tuliyomaliza jana usiku saa mbili usiku sa mbili nao tayari imetiwa saini, naomba niwajulishe wabunge kwamba miswada hiyo imepatiwa kibali na Rais," alisema.

Alisema kutokana na kupewa kibali na Rais na sasa ni sheria na kusisitiza kazi yote imefanyika kama zilivyopangwa na hakuna kiporo.

Ndugai alisema tangu Novemba 20, mwaka 2015 Rais alipozindua Bunge kazi nyingi zimefanyika ikiwamo miswada 60 kupitishwa na kupata kibali na kuwa sheria halali za nchi.

"Maazimio ni 38 yamepitishwa na Bunge la 11, maswali ya msingi yaliyoulizwa serikalini na wabunge na kupata majibu ni 3376, na maswali kwa Waziri Mkuu 172," alisema.

Pia, alisema Bunge hilo liliunda kamati nne za ushauri ikiwamo ya masuala ya Tanzanite, almasi, gesi asilia na uvuvi wa bahari kuu.

"Tumefanya kazi, tumetenda kazi Mheshimiwa Rais, wabunge hawa wametumikia Watanzania kwa uaminifu mkubwa sana wamenipa ushirikiano mkubwa sana na mimi kwa niaba yao, kuna wakati bunge linachemka kama bahari hadi tunakuudhi kidogo, lakini katika mchakato huu wa mambo ya kibunge yalivyo na ukumbi huu ni wa minyukano lakini yote ni mema," alisema.



Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu (kushoto), akikabidhi mpango mkakati wa tume hiyo wa mwaka 2018/23 kwa Waziri wa Afya wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hamad Rashid Mohammed baada ya mazungumzo, mjini Unguja Zanzibar jana. **PICHA: MAELEZO**.

# JPM: Kilichofanyika miaka 5 hiki hapa

## • Watumishi 32,500 watumbuliwa

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

RAIS John Magufuli amebainisha mafanikio ya serikali kwa miaka mitano ya uongozi wake, akibainisha kuwa ameajiri watumishi wapya 74,173.

Akilihutubia kwa mara ya mwisho Bunge la 11 bungeni jijini hapa kabla ya kulifunga jana, Rais Magufuli alisema kuwa miongoni mwa mafanikio hayo ni kudumisha amani na muungano, akieleza kuwa hilo limefanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Kiongozi huyo wa nchi alisema serikali imetatua kero nyingi za muungano na kumaliza tatizo lililoibuka mwanzoni mwa uongozi wake la mauaji dhidi ya viongozi na askari polisi katika wilaya tatu za Rufiji, Kibiti na Mkuranga mkoani Pwani.

Aliongeza kuwa wamefanikiwa kulinda mapinduzi matukufu ya Zanzibar na nchi imeendelea kuwa kisima cha amani na mipaka yake ni salama kutokana na kazi kubwa inayofanywa na vyombo vya ulinzi na usalama.

"Muungano wetu umeendelea kuimarika tumeshughulikia baadhi ya changamoto za muungano na kufikia makubaliano ikiwamo gharama za kushusha mizigo, kufuta tozo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na malimbikizo ya kodi ya Sh. bilioni 22.9 ambazo ZECO (Shirika la Umeme Zanzibar) ilikuwa ikidaiwa na Tanesco," alisema.

Alivipongeza vyombo vya ulinzi na usalama kwa kusimamia amani ya nchi na kueleza kuwa ripoti ya Global Peace Index ya Mwaka 2020 inaonyesha Tanzania imeshika nafasi ya kwanza Afrika Mashariki na ya saba kusini mwa Jangwa la Sahara kwa kuwa na amani.

Rais Magufuli alisema mafanikio mengine ya uongozi wake Ikulu ni kuimarisha maadili, nidhamu na utendaji serikalini, akibainisha kuwa katika kusimamia suala hilo, watumishi 32,555 wametumbuliwa.

Kati yao, 15,508 ni waliobainika kuwa na vyeti za kughushi na kwamba serikali yake pia ilibaini watumishi hewa 19,708 waliokuwa wanaigharimu Sh. bilioni 19.8 kila mwezi kupitia mishahara.

Alisema kuwa baada ya kutatua tatizo hilo la vyeti feki na watumishi hewa, serikali yake iliajiri watumishi wapya 74,173 na kuwapandisha vyeo watumishi 306,917, huku ikilipa deni la Sh. bilioni 472.6 kwa watumishi waliokuwa wakiidai.

"Tulichukua hatua zote hizo ikiwamo kutovumilia uzembe na kuhakiki vyeti vya watumishi ili kulinda heshima ya wafanyakazi," Rais Magufuli alisema.

Aliyataja mafanikio mengine kuwa ni vita dhidi ya rushwa na ufisadi, akieleza utendaji wa Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, maarufu Mahakama ya Mafisadi iliyoanzishwa mwaka 2016 na tayari imepokea mashauri 407 na kuyatolea uamuzi mashauri 385.

Alizungumzia pia utendaji wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) ambayo imefanikiwa kuokoa mabilioni ya shilingi na kuiwezesha serikali kutaifisha mali ikiwamo madini, nyumba, fedha za kigeni na hoteli ikiwamo ya jijini Mbeya.

Rais Magufuli alisema mafanikio yamepatikana pia katika kupunguza uingizaji wa dawa za kulevya nchini kwa asilimia 90, akibainisha kuwa kumechochewa na kutungwa kwa sheria nzuri, hivyo kuwapongeza wabunge kwa kazi nzuri na Watanzania kwa kutoa ushirikiano.

Alisema serikali yake pia imetatua tatizo la kukatika kwa umeme ambapo katika kipindi cha miaka mitano, nchi haikuwahi kuingia gizani.

Kwenye ukusanyaji mapato, Rais Magufuli alisema wastani wa ukusanyaji umeongezeka kutoka Sh. bilioni 850 mwaka 2014/15 hadi Sh. trilioni 1.3 mwaka 2018/19 huku bajeti ya maendeleo ikipanda kutoka asilimia 26 mwaka 2014/15 hadi 40 mwaka 2018/19.

Rais pia alisema wamefanikiwa kudhibiti matumizi serikali kwa kuzuia safari za nje, udanganyifu kwenye ununuzi na kupunguza idadi ya wizara kutoka 29 hadi 22. Pia rufani za matibabu ughaibuni nazo zimepungua kwa asilimia 95.

Vilevile, alisema hatua ya kuzimwa kwa mitambo ya kuzalisha umeme wa mafuta IPTL, Aggreko na Symbion imeokoa Sh. bilioni 716 kwa mwaka na kuiwezesha Tanesco kujiendesha yenyewe.

Pia, alisema wameboresha usikivu wa simu kutoka asilimia 79 mwaka 2015 hadi asilimia 94 mwaka 2019. Pia idadi ya watumiaji wa simu na data imeongezeka.

"Hii imechangiwa na kupungua kwa gharama za kupiga simu kwa dakika kutoka Sh. 267 mwaka 2014/15 hadi Sh. 40 sasa hivi," Rais Magufuli alisema.

Alisema mafanikio zaidi yamepatikana katika sekta za maji (miradi 1,423 imetekelezwa ikiwamo 1,268 ya vijijini); uchukuzi (kwa kununua ndege mpya 11 na kurejesha usafiri wa treni Dar-Moshi-Arusha, huku Zanzibar wakinunua meli mpya mbili); ujenzi wa barabara hasa zinazounganisha Mkoa wa Kigoma.

Sekta nyingine ni madini kwa kuanzisha wizara mahususi ya madini na masoko ya madini kila mkoa; nishati (ujenzi wa bwawa la Nyerere ili kuzalishaji MV 2115); utalii (kuongeza hifadhi tano mpya za taifa); na shughuli za serikali kuhamia Dodoma.

Mafanikio mengine ni kuimarisha vyuo vya ufundi na vya Tehama; kuimarisha utendaji wa mahakama; kutoa vitambulisho vya wajasiriamali, kutatua migogoro ya ardhi; kupaisha Kiswahili kimataifa; na kulipa madeni ya serikali kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

Rais Magufuli aliapishwa kuwa Rais wa Tanzania Novemba 5, 2015, akichukua mikoba ya Rais wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, baada ya kutangazwa mshindi wa kiti hicho katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 25, 2015 uliokuwa na ushindani mkali.

# Wanafunzi 100 wapata mimba kipindi cha corona

**Na Elizabeth Zaya**

ZAIDI ya wanafunzi 100 wamepata ujauzito katika kipindi cha miezi mitatu tangu ugonjwa wa corona uripotiwe nchini, Machi 16, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kuongezeka kwa mimba za utotoni ni sababu inayochangia kurudishwa nyuma watoto kielimu na kijamii.

Pia katika kipindi hicho cha mlipuko wa ugonjwa wa huo, kesi nyingi za ndoa za utotoni zimeendelea kuripotiwa kwenye vyombo vya habari.

"Mwaka 2018 na 2019, LHRC kilipokea taarifa ya zaidi ya kesi 2,540 za mimba za utotoni, hali hii imekuwa mbaya zaidi katika kipindi cha mlipuko wa ugonjwa wa corona kwa kuwa kwa miezi mitatu tu, zaidi ya wanafunzi 100 wamepata ujauzito na kesi nyingi za ndoa za utotoni zimeendelea kuripotiwa katika vyombo vya habari," ilieleza taarifa hiyo ya LHRC.

Kwa mujibu wa kituo hicho, matukio mengine ambayo yameendelea kuhatarisha usalama kwa watoto wa kike ni pamoja na walimu kubaka watoto wa kike na kuwasababishia ujauzito.

LHRC wanasema usalama wa watoto wakiwa shuleni umekuwa ukihatarishwa zaidi na walimu kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi wa kike na kuwasababishia ujauzito na kwamba mwaka 2018 hadi 2019, kituo hicho kilipokea kesi 24 za walimu waliokuwa na uhusiano na wanafunzi.

Kilitaja matukio mengine kuwa ni kuongezeka kwa ukatili wa kingono kwa watoto hao na kwamba mwaka 2019, taarifa ya Jeshi la Polisi na za LHRC zilionyesha kwamba ukatili huo kwa watoto ukiwamo wa ubakaji na ulawiti unazidi kuongezeka.

"2019 Januari hadi Juni mwaka huo, kesi 126 ziliongezeka ukilinganisha na mwaka 2018 ambapo vitendo vya ulawiti vilivyoripotiwa vilikuwa 141," ilisema taaifa hiyo ya LHRC.

"Kwa ujumla, kuanzia mwaka 2016 hadi 2019, Jeshi la Polisi limepokea kesi zaidi ya 42,824 na kuna kesi nyingi ambazo haziripotiwi. Katika utafiti wa mtandaoni wa LHRC, asilimia 84 ya kesi zilizopokelewa ni ukatili wa kingono kwa watoto."

Matukio mengine kilisema ni ukatili wa kimwili kwa watoto hao, maambukizi ya virusi vya Ukimwi, ajira za watoto, watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani na walio na migogoro na sheria.



Meneja Msaidizi wa Idara ya Ukaguzi na Sera Benki Kuu ya Tanzania, Albert Cesari (wa nne kulia), akiwa na watendaji wakuu wa kampuni ya Vodacom Tanzania PLC, baada ya kuzindua huduma mpya ya kutuma na kupokea pesa kutoka nchi zaidi ya 200 duniani kupitia mtandao wa M-Pesa iitwayo Dunia ni Kijiji na M-Pesa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Mchungaji mbaroni kwa tuhuma rushwa

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Kagera, inawashikilia watu sita kwa makosa ya kuomba, kupokea na kutoa rushwa akiwamo mchungaji wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Biharamulo.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapa, John Joseph, alisema watuhumiwa hao walitenda makosa kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007 chini ya kifungu cha 15(1)(a)(b).

Alisema Juni mwaka huu majira ya jioni taasisi ilipokea taarifa kutoka Jeshi la Polisi wilayani Biharamulo ya kumkamata Diwani wa Kata ya Nyarubungo, Furgence Zamkobaho na mkewe, Ana Jeremiah ambaye ni muuguzi wa Hospitali teule ya Wilaya ya Biharamulo.

Alisema watuhumiwa hao walikuwa wanashikiriwa kwa kosa la kukutwa wakiuza dawa tiba katika duka la dawa zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kuhudumia wananchi.

Alisema, mtuhumiwa namba tatu ambaye ni mchungaji, Zakaria Kaigarula, alifika katika kituo cha polisi ambako walikuwa wameshikilia Zamgobaho na mkewe Jeremia kwa ajili ya kutoa hongo kwa polisi ya shilingi milioni moja ili kusamehewa.

"Mchungaji huyo baada ya kuhojiwa na taasisi alikiri kutumwa na watuhumiwa kwamba awatolee rushwa ili wasamehewe makosa ndipo alibainika kuwa na kosa la kula njama kwa Sheria ya Kifungu cha 15(1)(b) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007," alisema Joseph.

Alisema watuhumiwa wengine ni Mtendaji wa Kata Ibuga wilayani Muleba, Mhidini Mudricati ambaye Juni 6, mwaka huu aliomba rushwa ya shlingi 50,000 kwa mwananchi aliyemkamata na pombe haramu aina ya gongo ili asimchukulie hatua.

Mwingine ni Edna Magazi, Ofisa wa Wakala za Misitu (TFS), ambaye anadaiwa kuomba rushwa ya shilingi 100,000 kutoka kwa mwananchi aliyemkamata na gunia la moja la mkaa.

# Adaiwa kujinyonga hadi kufa kwa waya wa umeme

**Na Lilian Lugakingira,**

BUKOBA

MWENDESHA pikipiki Ishengoma Rafael (29), mkazi wa kitongoji cha Kyasha Bukoba Vijijini, mkoani Kagera, anadaiwa kujinyonga hadi kufa kwa kutumia waya wa umeme, ndani ya chumba alimokuwa akiishi.

Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revocatus Malimi, alisema kuwa kijana huyo anayefanya kazi ya bodaboda alirejea nyumbani Juni 14, mwaka huu saa mbili asubuhi akitoka katika shughuli zake na alipoingia ndani hakutoka mpaka muda wa saa 10 jioni, majirani walipoamua kugonga mlango.

"Majirani walipoona hafungui walitoa taarifa katika uongozi wa serikali za mitaa ambao walichukua jukumu la kufungua mlango wa chumba chake na kukutwa akiwa tayari amefariki dunia," alisema.

Alisema, kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na kaka yake (jina halikufahamika) kwa jeshi hilo, kijana huyo alianza kuonyesha dalili tofauti tangu Juni 8, mwaka huu, alipokwenda nyumbani kwa ndugu yake huyo na kumweleza kuwa hajisikii vizuri.

"Alimwambia kaka yake kwa kuwa hajisikii vizuri anaomba kulala kwake, akamkubalia, lakini usiku wakati amelala alisikika akiongea mwenyewe huku akitoa maneno ya kulaumu, lakini alipoulizwa ana tatizo gani hakusema na kumuahidi kaka yake kuwa angemweleza siku nyingine," alisema.

Kamanda Malimi alisema kuwa walipoamka asubuhi kila mmoja aliondoka kwenda katika shughuli zake na hakuonana tena na kaka yake hadi alipopigiwa simu na majirani, wakimtaarifu kuwa mdogo wake amejinyonga.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, uchunguzi wa kifo hicho unaendelea.

HABARI KITAIFA

# Wamiliki shule waja na maagizo

Na Waandishi Wetu

BAADA ya Rais John Magufuli, kutangaza kuzifungua shule zote ifikapo Juni 29, baadhi ya wamiliki wa shule wametoa masharti kwa wazazi kuwa barakoa zitakazoruhusiwa ni zile zitakozotengenzwa shuleni.

Rais Magufuli alitoa tangazo hilo wakati wa kulifunga Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jana jijini Dodoma, akisema kuwa kutokana na kupungua kwa maambukizi ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu (Covid-19) unaotokana na virusi vya corona, lazima maisha yaendelee ikiwamo kufungua shule na shughuli nyingine za kijamii.

Baadhi ya makundi songezi (WhatsApp) yaliyounganisha uongozi wa shule na wazazi, zimetoa malekezo kwa wazazi ya namna watoto wanavyotakiwa kurejea shuleni kwa kuchukua tahadhari dhidi ya corona.

Moja ya shule binafsi ya jijini Dar es Salaam, imeandika ujumbe mfupi kwa wazazi kuwaeleza kuwa watoto watakaporejea shuleni watatakiwa kuvaa barakoa zitakazotengenezwa na shule na si vinginevyo.

Mmoja wa wazazi wa shule hiyo, aliliambia gazeti hili kuwa wanahitaji serikali itoe mwongozo wa afya pamoja na huduma nyingine ikiwa ni pamoja na ada ambazo baadhi yao wamelipa hadi mwezi Juni.

"Mwanzoni mwa mwezi huu shule anayosoma mwanangu tulitumiwa ujumbe kwenye kundi la WhatsApp kujulisha kuwa shule imefungwa mpaka Julai 6, baada ya muhula wa kwanza kuisha.

"Tumeambiwa muhula wa kwanza umeisha kwa sababu watoto walikuwa wanatumiwa kazi za nyumbani kupitia mtandao. Tunaomba serikali iliangalie suala hili kwa sababu siyo watoto wote ambao walishiriki masomo hayo."

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Sylvia Lupembe, alisema wizara ya elimu itaandaa mwongozo ambao unatarajia kutolewa leo.

Jana, Rais Magufuli wakati akivunja Bunge, jijini Dodoma, pamoja na mambo mengine alitangaza kuzifungua shule zote ambazo awali zilifungwa kutokana na ugonjwa wa corona.

Ufunguaji wa shule na vyuo umekuwa ni mwendelezo baada ya Mei 21, Rais Magufuli kutangaza kufungua kidato cha sita.

**NDALICHAKO AKIFUNGUKA LEO**

Wakati huo huo, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof.Joyce Ndalichako, amesema kutokana na uamuzi wa Rais Magufuli wa kufungua shule Juni 29, mwaka huu, leo atazungumza na Watanzania.

Akizungumza nje ya Bunge na waandishi wa habari, Prof. Ndalichako alisema hatalala usingizi hadi aandae ratiba ya mtihani wa darasa la nne, saba na kidato cha nne.

Prof. Ndalichako alisema: "Huu uamuzi nilikuwa nausubiri kwa hamu na kesho (leo) nitazungumza na Watanzania utaratibu utakuwaje baada ya Rais kutangaza ili wamiliki wa shule na wanafunzi wajipange."

Aliwataka wazazi kujiandaa kuanza kurudisha watoto wao shuleni.

**Imeandikwa na Romana Mallya, DAR na Agusta Njoji, DODOMA**

# Mbowe ajitosa urais, afunguka

Na Elizabeth Zaya

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema hakutarajia kutia nia ya kugombea urais isipokuwa aliamua kufanya hivyo kwa kutii ombi la wazee wa chama chake waliomshawishi kufanya hivyo.

Juzi Juni 15, ikiwa ndiyo siku ya mwisho ya chama hicho kufunga dirisha la watia nia katika nafasi hiyo ya urais kupitia CHADEMA, wazee wa chama hicho, walimfuata Mbowe na kumuomba atie nia katika nafasi hiyo.

Kwa mujibu wa Mbowe, aliamini kwamba watia nia ambao wamekwishajitokeza kutia nia hiyo mpaka Juni 15, kupitia chama hicho walikuwa ni wagombea wazuri.

"Sikukusudia kutia nia katika nafasi ya kugombea urais, sio kwa sababu siwezi ila ni kwa sababu ninaamini katika kutumia muda wangu zaidi kujenga taasisi, kukijenga chama na kunyanyua vipaji vya uongozi miongoni mwa vijana, wazee, kinamama na hata wasichana miongoni mwao," alieleza Mbowe.

"Wagombea ambao wameshajitokeza mpaka hatua ya sasa, nina imani kabisa ni wagombea wazuri, ni wagombea bora na bado nina imani wapo wagombea wengine wengi ambao ni bora."

"Nimekitumikia chama hiki tangu kimezaliwa kwa unyenyekevu na uadilifu mkubwa kwa zaidi ya miaka 30. Umri wangu ni chama hiki, muda wangu wote wa ujana nimeutumia katika harakati."

Mbowe alisema wote walio tia nia hiyo kupitia chama hicho, watapimwa na kuhakikisha anapatikana mmoja mwakilishi ambaye atatakiwa kuwaunganisha wote.

Alisema hatakubali wala kuruhusu katika hatua yoyote ya sasa ikaleta mgawanyiko ndani ya chama hicho.

"Natambua wako ambao wametangaza nia hadharani na ambao hawajatangaza hadharani, lakini wamewasilisha barua zao za makusudio kwa Katibu Mkuu, wote hawa ni wa kwetu, na wote chama kwa kutumia mifumo yake itawapima na kuhakikisha mwisho wa siku anapatikana mwakilishi ambaye wote waliotangaza nia watamuunga mkono," alisema Mbowe.

"Mimi Mwenyekiti sitakubali na sitaruhusu katika hatua yoyote ya sasa, chama hiki tukagawane makundi ya wagombea wa urais. Hatua ya kujitokeza wagombea wengi ni hatua za awali za kuwezesha ndoto za kila mmoja wetu kutimia."

"Yawezekana ukawa na ndoto hiyo, wenzako wakakuambia bado kidogo usubiri, kwa hiyo yeyote ambaye hatimaye atatolewa kama chaguo la chama, wajibu wake mkubwa sio kupeperusha bendera ya kundi lake, ni kuunganisha wote wale waliogombea hatimaye wataungana pamoja na wale ambao hawakugombea ili twende katika uchaguzi wa Oktoba tukiwa chama kamili, imara na chenye mshikamano."

Mbowe alisema pamoja na wazee hao kumpendekeza atie nia katika nafasi hiyo ya urais, lakini lazima chama kitaheshimu na kusimamia msimamo wa chama kwa kumchagua mgombea bila kujali nafasi yake ndani ya chama hicho.

"Pamoja na nyie kunipendekeza, mwisho wa siku chama hiki lazima kikaamue nani akawe mgombea wetu, kwa mazingira ya kawaida, namba moja ya mgombea angekuwa mwenyekiti, lakini miaka yote nimekataa utawala huo," alisema na kuongeza:

"Nimesema yeyote tunayefikiri anaweza kufanya, apewe nafasi bila kujali ana cheo kikubwa kiasi gani ndani ya chama hata mwanachama wa kawaida ukiwiwa kugombea urais, unaweza kutia nia."

Mbali na Mbowe, makada wengine wa CHADEMA ambao wameshatangaza nia ya kuwania uteuzi wa urais ni Mbunge wa Iringa Mjini, Mchungaji Peter Msigwa, Lazaro Nyalandu, Makamu Mwenyekiti Tanzania Bara, Tundu Lissu na Dk. Maryrose Majinge.



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Felix Lyaniva, akizungumza na wawezeshaji watakaoenda mitaani kuwahakiki walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF), wakati akifungua mafunzo kwa wawezeshaji hao, katika Manispaa ya Temeke, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Ofisa Tarafa ya Mbagala, Betha Minga, na Kaimu Meneja Uhawilishaji Fedha wa TASAF, Seleman Masala. **PICHA: JUMANNE JUMA**


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **RIMBO AUCTION MART na WANGWANA AUCTION MART** kwa niaba ya AccessBank Tanzania Limited watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba, Magari na Viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili, Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | LUMUMBA | RIMBO COMPANY LIMITED | AROT/W,NICKSON | AROT/W,NICKSON | KIWANJA | NAKALEKWA/NAKASANGWE (WAZO) | 30/06/2020 SAA 4:00ASUBUHI |
| 2 | KIJITONYAMA | WAUNGWANA AUCTION MART | SWAI/AROBOGAST,CHARLES | SWAI/AROBOGAST,CHARLES | KIWANJA | GOBA MATOSA | 29/06/2020 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 3 | LUMUMBA | RIMBO AUCTION MART | MWALUMU/IZACK,TAMIKA | MWALUMU/IZACK,TAMIKA | NYUMBA | TABATA | 29/06/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. UKAGUZI UNARUHUSIWA MARA USOMAPO TANGAZO HILI.
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA MALIPO YA 25% YA FEDHA TASLIMU PAPO HAPO NA 75% BAADA YA SIKU 14 TOKA SIKU YA MNADA KUFANYIKA NA UKISHINDWA KULIPA MALIPO YALIYOBAKI MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZO LIPA HAZITARUDISHWA
3. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE, KUMBUKA VIGEZO NA MASHARTI KUZINGATIWA.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**
**RIMBO COMPANY LIMITED 0712848820**
**WAUNGWANA AUCTION MART 0713077474**
**WOTE MNAKARIBISHWA.**

215777202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# 2020 tuachane na wabunge mizigo

**BUNGE** limevunjwa na sasa ni rasmi kuwa Taifa linaelekea kwenye mchakato wa uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Wabunge, madiwani na watia nia wengine wanarudi majimboni kwenye wapigakura kuanza mchakato wa kujinadi na kujieleza jinsi walivyofanya kazi ya kuwatetea na kuwasemea kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Tunaamini kuwa katika mfumo wa kidemokrasia uwakilishi ni lazima kwa vile sisi Watanzania milioni 50 hatuwezi kwenda bungeni, kwa hiyo wabunge wetu tunaowapigia kura ndiyo wanaotuwakilisha.

Ndiyo maana tunahimizana kuchagua viongozi wawajibikaji, wazalendo, wachapakazi na waadilifu kwa kuwa ndiyo watetezi wetu na ndiyo watakaoibana na kuisimamia serikali kuchukua hatua kutatua matatizo yetu wapigakura.

Tunafahamu fika kuwa ndiyo watetezi wa wapigakura wao walioko mijini, vijijini na kwenye majiji katika masuala yote yanayohusu ustawi wa jamii.

Tunapolitizama hilo tunategemea kuwa wananchi kuanzia sasa watachagua wabunge wanaotimiza wajibu wanaobadilisha hali za watu kwa kutimiza jukumu lao la kuisimamia serikali ili wahakikishe inawajibika kwa wananchi.

Ndilo daraja lililoko mstari wa mbele kuisimamia serikali ili itimize wajibu wa kuwahudumia wananchi kwa kufanyakazi kwa misingi ya sheria na katiba kwenye kusimamia miradi ya maendeleo na matumizi ya fedha za walipakodi.

Ni watu wa kuhakikisha kuwa masuala ya wapigakura yanakuwa ya muhimu na yanapewa kipaumbele na hatua kuchukuliwa kwa wakati ili kutatua kero za wananchi.

Wabunge ndiyo ambao kwa kuisimamia serikali watasaidia kuondoa umaskini, ujinga na maradhi katika majimbo yao.

Kwa hiyo, tunapoelekea kwenye uchaguzi mkuu tunawaomba wapigakura kuwa makini na mienendo ya wabunge watarajiwa kwa kuwahoji kuhusu masuala ya maendeleo kwenye mitaa, miji, majiji na vijijini kwa kuangalia walichofanya.

Tungependa kufahamu wabunge wanaoondoka wamesaidiaje kuendeleza wapigakura kwa kutumia fedha za mfuko wa maendeleo ya jimbo?

Wamewasaidiaje wapigakura kutatua changamoto za muda mrefu kama ukosefu wa zahanati, madarasa, nyumba za walimu, maji, vyoo shuleni kwa muda wa miaka mitano?

Wagombea hao wanaotaka tena kuwa wabunge kama waliokuwa wabunge au madiwani wanaomaliza muda wao, wamebadilishaje maisha ya wahitaji wakiwamo wanawake, wajane, mabinti na wale wenye mahitaji maalumu?

Tunasema haya kwa sababu tunahitaji viongozi wawajibikaji na si kwenda bungeni kwa ajili ya kupata na kutumia mfuko wa jimbo, kiinua mgongo na posho za kila siku, huku madiwani nao wakivizia posho za vikao na kiinua mgongo.

Ikumbukwe kuwa miaka ya nyuma hamu ya madaraka ilisababisha wabunge na madiwani wenye fedha kununua uongozi ili kujipatia nafsi hizo kwa lengo la kutimiza azma zao kama kupata zabuni kwenye halmashauri.

Hayo ni mambo ambayo yalisababisha mkanganyiko na kurudisha nyuma juhudi za maendeleo kwa kuwa walionunua uongozi ndiyo walionunua uongozi wa halmashauri, vijiji na hata madiwani ili kutimiza azma zao. Wabunge hao ndiyo waliotumia ujanja wa fedha kujipatia au kuwapatia jamaa zao au watu wa karibu zabuni za ujenzi wa majengo, kandarasi mbalimbali zikiwamo za miundombinu, ajira na nafasi mbalimbali ili kujinufaisha.

Hayo ni mambo yaliyoziangusha halmashauri na maeneo mengi kimaendeleo kutokana na fedha kuchangamkiwa na wabunge na madiwani na wenyeviti wa halmashauri wajanja.


Kwa hiyo tunapoelekea kwenye uchaguzi mkuu wa wabunge na madiwani hakuna haja ya kuendekeza wabunge na madiwani kama hao.

Tunategemea kuona wabunge na madiwani wanaochapakazi wakichaguliwa kuliongoza taifa kwenye uwakilishi wa wananchi bungeni na kwenye kata.

Shime wananchi ni wakati wa kutambua na kuchagua viongozi bora na si bora mbunge au diwani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Mary Geofrey

# Hongera CCM kudhibiti wanaonunua uongozi

**KUANZIA** sasa ni rasmi kuwa Chama Cha Mapinduzi kimepuliza kipenga cha kufungua milango ya wagombea urais wa Tanzania Bara na Visiwani.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole, anaitangaza ratiba ya mchakato huo na namna urais wa Tanzania Bara utakavyoanza na uchukuaji fomu.

Pamoja na ratiba iliyotolewa na CCM, chama hicho kinatoa masharti kwa wagombea na wanachama wenye nia ya kushiriki katika uchaguzi huo.

Kikubwa chama kimesisitiza wanachama kuwa watulivu na kusubiri ratiba ya uchaguzi badala ya kuanza kujipitisha mitaani kuomba kuungwa mkono badala yake wasubiri kupitishwa kwa mujibu wa katiba ya chama hicho.

Chama hicho kimetoa tahadhari kwa washiriki wa ugombea wa nafasi hizo kuwa wanyenyekevu na kutojihusisha na rushwa wakati wakisubiri kuteuliwa.

Katika kuhakikisha wanadhibiti vitendo vya rushwa, chama hicho kinaweka bayana kuhusu kikao walichoketi na Mkurugenzi wa Taasisi ya Kuzuia naKupambana na Rushwa (Takukuru), Brigedia John Mbungo, kuandaa mikakati ya kushirikiana kuwakamata wagombea watakaojihusisha na mlungula.

Kwa mujibu wa Polepole, watakaojihusisha na rushwa watakatwa majina na hawatapata nafasi ya kuwania kupitia CCM wala vyama vingine vya siasa.

Tahadhari zilizotolewa na CCM ni jambo jema na linalopaswa kusimamiwa kikamilifu ili kudhibiti rushwa wakati wa uchaguzi.

Tumekuwa tukishuhudia katika chaguzi zilizopita wagombea wakitoa fedha kwa wanachama na viongozi wa juu ili majina yao yapitishwe na kushiriki katika uchaguzi.

Na matokeo ya hayo ni kupatikana kwa viongozi wasiyo na sifa wala wito wa kutumikia wananchi na badala yake kuwa ni viongozi wenye maslahi binafsi ya kujilimbikizia mali na waroho wa madaraka.

Ni hatua nzuri za mfano wa kuigwa zilizochukuliwa na CCM katika hatua za awali kabisa kabla ya kuanza mchakato ili kupunguza au kumaliza vitendo vya rushwa nchini.

Kwa CCM walichokianzisha ni cha kishujaa kinachotakiwa kutekelezwa kwa vitendo ngazi zote.

Ni jambo la kizalendo na la mfano wa kuigwa na vyama vingine vya siasa kuanza kukemea rushwa wakati bado mchakato ukiwa katika hatua za awali badala ya kusubiri Takukuru kuingilia kati.

Ni muhimu vyama vya siasa kuwa mfano wa kuigwa katika kushiriki kupambana na vitendo vya rushwa kwa sababu moja ya eneo ambalo limekithiri kwa rushwa ni kwa wanasiasa wakati wa uchaguzi.

Kila kiongozi akitambua kuwa haki na uongozi siyo bidhaa ya kununuliwa na wakapitisha wenye sifa na siyo wenye fedha kama ambavyo CCM imeanza kufanya. Ni wazi kuwa wenye nia ya kununua uongozi watashindwa kutimiza lengo hilo.

Mapambano dhidi ya rushwa yanaanza na wewe mwenyewe na siyo kusubiri kuonywa au kukamatwa.

Kwa upande wa ratibu wana CCM wanaambiwa kuwa kuanzia Juni 15 hadi 30 mwaka huu ni kuchukua fomu sambamba na utafutaji wa wadhamini mikoani.

Polepole anabainisha zaidi kuwa, baada ya mchakato huo kukamilika, kitakachofuata ni vikao vya uchukuaji majina ya wagombea, vitakavyoanza Julai 6 hadi 7 mwaka huu.

Ratiba hiyo inakwenda sambamba na ile ya Zanzibar ambayo itaanza Julai 15 hadi 30 ya kuchukua fomu na kutafuta wadhamini mikoani.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, Julai Mosi hadi 2, mwaka huu vitaanza vikao vya Sekretarieti ya Kamati Maalumu ya Halmashauri Kuu ya Taifa Zanzibar.

Julai 3, mwaka huu kitakaa kikao cha Kamati ya Usalama na Maadili Zanzibar, ratiba itakayofuata ni Kikao cha Kamati Maalumu ya Halmashauri Kuu ya CCM, kitakachokaa Julai 4, mwaka huu, kwa ajili ya kutoa mapendekezo juu ya wanachama waliojitokeza kuomba kugombea urais wa Zanzibar.

Kadhalika kwa vyama vingine vya siasa navyo vimeanza kuweka wazi ratiba za mchakato wa kuwania nafasi za uongozi kupitia vyama husika, kabla ya kuelekea uchaguzi mkuu Oktoba mwaka huu.

## W'biashara Mwanza wahamasishwa kulipa kodi

**Na Magdalena Haule,** UDOM

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, amewataka wafanyabiashara kutumia fursa ya kampeni ya elimu kwa mlipakodi inayoendelea, ili kulipa kodi kwa wakati na kuiwezesha serikali kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kampeni ya elimu ya mlipakodi ilianza juzi na inatarajiwa kumalizika Juni 22, mwaka huu, mkoani humo.

Mongella alitoa wito huo juzi akizungumza na wananchi wa mkoa huo wakati wa ufunguzi wa kampeni hiyo na kuwataka wafanyabiashara kulipa kodi kwa wakati, ili kuiwezesha serikali kugharamia huduma za kijamii.

"Kama mnavyojua umuhimu wa kodi, hakuna Mtanzania ambaye hajashuhudia umuhimu wa ulipaji kodi kwa serikali hii kwa sababu tumeshuhudia barabara zikijengwa, ndege zikinunuliwa, ujenzi wa vituo vya afya, meli zikijengwa na ukarabati wa viwanja vya ndege, miradi ambayo imetekelezwa kwa mapato ya ndani," alisema Mongella.

Alisema kampeni hiyo imelenga kuwafikia wananchi na wafanyabiashara wa maeneo mbalimbali mkoani hapo, yakiwamo Rwagasore, Pamba Road, Buhongwa, Nyerere Road, Misungwi, Mwaloni na Kisesa.

Kwa upande wake, mfanyabiashara wa mapambo, Flora Ayo, na wa duka la vifaa vya ujenzi, Charles Lyamuya, waliomba kampeni ya elimu kwa mlipakodi kuwa ni endelevu kwa ajili ya kujenga ushirikiano kati yao na TRA.

"Kwa elimu tuliyoipata ni hakika tutalipa kodi ipasavyo kwa sababu inatuweka karibu na TRA suala ambalo linatuondolea hofu. Tunaomba iwe ni kampeni endelevu ili kuwajengea ujasiri wa kulipa kodi wafanyabiashara wote," alisema Lyamuya.

# Ndugai aeleza sababu kuwa na hasira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesimulia maisha aliyopitia wakati akisoma na jinsi alivyokuwa katika maisha ya umaskini mkubwa ikiwamo kulala njaa na kwamba hakuwahi kufikiria kushika nafasi hiyo.

Amesema kumaliza salama Bunge la 11, sifa apewe Bwana wa Majeshi (Mungu).

Akizungumza juzi bungeni baada ya kuhitimishwa shughuli za Bunge na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Spika Ndugai alisema katika maisha yake hakuwahi kuwaza, kuota au kufikiri kuwa mwanasiasa.

"Sikuwahi kuota kama siku moja nitakuwa mbunge, na kuwa Spika ndio kabisa, sikuwahi kufikiri hata mara moja, ni Mungu tu, Mungu wa ajabu ambaye katika uumbaji wake hutujua na kutupangia safari kadri anavyoona," alisema.

Alisema anakumbuka alivyokuwa akisoma shule ya msingi miaka ya 1970, Sagala Kongwa, akitokea kijijini kwao Laikala umbali wa kilometa nane.

"Kwa hiyo tulikuwa tunasoma siku tano kwa wiki na natembea kilometa 16 kwa siku, kwa siku tano ni kilometa 80, nimekulia maisha ya shida, dhiki na miaka mingine wakati wa njaa Dodoma nilipitia maisha hayo, nikiwa mdogo nililala kitanda cha kamba, ngozi ya ng'ombe na kuishi nyumba ya tembe na nilichunga sana ng'ombe."

"Baadaye nilikua kwa kudra ya Mwenyezi Mungu na kusoma vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi, lakini nakumbuka nilipokuwa Chuo cha Mweka Moshi, tulikuwa wanafunzi wa nchi mbalimbali Afrika, nilikuwa mmoja wa wanafunzi maskini sana chuoni."

"Baadhi ya likizo nilikuwa sina nauli ya kurudi Dodoma Kongwa, kwa hiyo tukakubaliana na Mkuu wa chuo wakati huo niwe nabaki natumikia tumikia pale kufyeka majani, kupanga vitabu na kusaidia walimu katika utafiti wa kukusanya data," alisema.

Alisema wakati wa likizo alilazimika kujificha ili kukwepa kuulizwa na wanafunzi wenzake kwanini harudi kwao.

Ndugai alisema alikuwa mtoto mmoja wa pekee kwa mama yake anatamani angekuwapo ampokee, lakini Mungu alishamchukua.

**AOMBA MSAMAHA WABUNGE**

Kutokana na maisha hayo, Ndugai aliomba wabunge wamsamehe wakati mwingine alipokuwa mkali kwao.

"Kwa hiyo wakati mwingine mnisamehe huwa napata hasira nikikutana na mtu mjinga, sisi tumeshapita huko tumeshapata tabu, huo ukamanda tumeshapitia kukanyaga kilometa 80 kwa wiki, wewe utakuwa kamanda kunizidi mimi kweli," alisema.

Kuhusu kumalizika kwa bunge hilo, alisema amekuwa akiulizwa na waandishi wa habari kuwa anajisikiaje kumaliza salama Bunge la 11: "Sifa apewe Bwana wa Majeshi".

Alisema miaka 20 ya maisha yake ameitumikia bungeni na amekutana na watu wengi wema sana na changamoto nyingi sana.

"Tunakaribia watu 400 ni wengi sana, mwalimu wangu aliwahi kusema darasa moja lina wanafunzi 40, na kati yao kuna watu wana tabia ya askofu, mufti, walevi, wezi...Hapa kati ya tabia za mwanadamu zote zipo," alisema.

Alibainisha kuwa imekuwa ni fadhila kwake kuhudumu kama kiongozi kwa miaka mitano na kuwashukuru wabunge kwa kumwamini.

**USHIRIKIANO NA RAIS**

Spika Ndugai alisema kuna wakati watu walikuwa wakimjaribu, lakini alikuwa alipata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa Rais John Magufuli.

"Kuna wakati watu walikuwa wakinijaribu labda niseme nilikuwa na 'strong support' ndio maana tumefika hapa leo, kwa hiyo namshukuru mno."




Wafanyakazi wa Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, wakichangia damu katika Hospitali ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru jana, kwa ajili ya kuiwezesha benki ya damu kuwahudumia wagonjwa kikamilifu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yakamata fulana zinazoashiria kampeni

**Na Emmanuel Lengwa,** SONGWE

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa Songwe imekamata na kuzuia fulana za Chama Cha Mapinduzi (CCM), zenye picha ya Rais Dk. John Magufuli na jina la Mbunge wa Jimbo la Songwe, Philip Mulugo, kwa madai kuwa zina maneno yanayoashiria kuanza kampeni za uchaguzi mkuu kabla ya wakati.

Akizungumza na Nipashe, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Songwe, Damas Suta, alisema waliamua kukamata na kuzuia ugawaji wa fulana hizo kwa wananchi wa Jimbo la Songwe baada ya kubaini kuwa ni kinyume cha sheria na kanuni za uchaguzi za CCM.

Suta alisema kazi ya mbunge ni kufanya shughuli za maendeleo na kuwasaidia wananchi katika changamoto zao na siyo kuanza kampeni kwa kutumia ugawaji wa fulana, huku akidai kuwa kitendo hicho ni kinyume cha Sheria za Uchaguzi ya CCM namba 16 na 17 za mwaka 2017.

"Tumekamata fulana hizo japo idadi yake siwezi kujua, na baada ya kuzikamata tumeamua kuzirudisha kwa Katibu wa CCM Wilaya ya Songwe ili azihifadhi mpaka wakati wa kipindi cha kampeni kitakapoanza," alisema Suta Kamanda wa Takukuru Songwe.

Akizungumzia fulana ambazo zilikuwa tayari zimekwishagawiwa kwa wananchi, Suta alisema kuwa hawezi kujua fulana hizo ziligawiwa kwa watu gani, ingawa wana uhakika kwamba ziligawiwa kwa watu na kwamba wao wajibu wao ni kuzuia ugawaji na uvaaji wa fulana hizo kwa vile muda wa kampeni haujafika.

Suta alisema mbali na fulana hizo kuwa na maandishi upande wa mbele, pia zina maandishi mengine upande wa nyuma ambayo yanasomeka 'JPM 2020 TENA Papa Mulugo Ahadi umepata 2015-2020'.

Alisema Takukuru wanaendelea kuzisaka fulana nyingine ambazo tayari zimeshagawiwa kwa wananchi ili wazikusanye na kuzirejesha kwenye ofisi za chama kwa lengo la kuzuia watu kuanza mapema kampeni za uchaguzi.

Alisema baada ya kukamata na kusimamisha zoezi la ugawaji wa fulana hizo, Takukuru pia walitoa taarifa kuhusu uamuzi huo kwa viongozi wa CCM wa wilaya akiwamo mwenyekiti na katibu.

Suta alisema, pia Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashilu Ally alisema mwaka huu chama hakitagawa bure fulana, bali wanachama watatakiwa kuzinunua, hivyo kitendo cha mbunge huyo kugawa fulana bure ni kukiuka agizo la Katibu Mkuu.

Akizungumza sakata hilo Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Songwe, Mwalimu Hamad Juma, alikiri kupokea taarifa za kukamatwa na kurejeshwa kwa fulana na kwamba hata yeye bado hajaziona.

# Mnada wawapa neema wakulima wa ufuta, soya

**Na Gideon Mwakanosya,** RUVUMA

MNADA wa nane wa mazao ya ufuta na soya ulioshirikisha halmashauri tano za mkoa wa Ruvuma na vyama vya msingi vya ushirika 11 umewawezesha wakulima kuuza zaidi ya kilo 264,000 za ufuta na kupata zaidi ya Sh. milioni 400.

Akizungumza baada ya mnada huo katika soko la mazao la Lilambo, Meneja Operesheni wa Chama Kikuu cha Ushirika wa mazao ya kilimo Songea na Namtumbo (SONAMCU), Zamakanary Komba, alizitaja halmashauri tano zilizoshiriki katika mnada huo ni Mbinga, Songea, Madaba na Nyasa.

Alisema bei ya juu iliyokubalika na wakulima ilikuwa ni Sh.1,930 na baada ya kutoa tozo mkulima anauza kwa Sh.1,759.

"Pesa ambayo imekwenda moja kwa moja kwa wakulima katika mnada wa leo ni Sh. 465,250,223, lakini kabla ya makato kwenda kwa wakulima, fedha ilikuwa ni zaidi ya shilingi milioni 510," alisisitiza Komba.

Komba alisema kupitia mnada huo, tozo ya mfuko wa maendeleo katika halmashauri zimepatikana Sh. milioni 7.9, na kwamba ushuru wa halmashauri ni zaidi ya Sh. milioni 20.6.

Aidha, alisema mnada wa zao la soya umeshirikisha halmashauri mbili, na kwamba wakulima wamegomea bei ya zao hilo ambayo bei ya juu ilikuwa ni Sh. 680 kwa kilo, ambapo ukitoa tozo mkulima alikuwa anabakiwa na Sh. 558.

"Kutokana na hali hiyo, tumeusogeza mbele mnada huo hadi Jumatatu ijayo, leo tuliangalia asubuhi bei ya Dar es Salaam ilikuwa kilo ni Sh. 800, Morogoro Sh. 850 kwa hiyo tunawashauri wenye kampuni wanunue bei nzuri kutoka kwa wakulima," alisisitiza Komba.

Wakulima wa ufuta kwa wilaya za Namtumbo, Songea na Tunduru mkoani Ruvuma wameanza kunufaika na zao hilo baada ya kupokea Sh. bilioni 16.8 tangu kuanza kuuza zao hilo kwa mfumo wa stakabadhi ghalani Aprili 30, mwaka huu.




Ofisa Msimamizi Mkuu wa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Maternus Mallya (kulia), akimwelimisha mlipakodi kuhusu umuhimu wa utunzaji wa kumbukumbu za biashara wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi, inayoendelea mkoani Morogoro, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# CCM waonywa kuhusu rushwa

**Na Jumbe Ismailly SINGIDA**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Singida Mjini kimewatahadharisha wanachama wake wenye nia ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi mkuu ujao, kujiepusha na vitendo vya kutoa rushwa kwa wapigakura.

Katibu Mwenezi na Siasa wa Chama hicho, Jumanne Nkii, ametoa tahadhari hiyo kwenye hafla ya uzinduzi wa shina la wakereketwa la wajasiriamali Ginery katika Kata ya Mandewa pamoja na kumpokea aliyekuwa diwani wa Kata ya Mandewa kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Shabani Kiranga.

Aliwataka wanachama wa chama hicho kutotumia kipindi cha uchaguzi kwa kuchafuana, kupakana matope badala yake watumie nafasi ya kikatiba ya kukubali matokeo baada ya kutangazwa.

"Kama utacheza vizuri, ukacheza ndani ya mchakato kwa njia zinazotakiwa utakwenda salama, lakini kikubwa ndugu zangu tusijihusishe na rushwa, tusichafuane, tusipakane matope ninaomba kila mmoja atumie nafasi yake ya kikatiba kuomba kugombea," alisema.

Aliwaonya wanachama wenye nia ya kugombea wasiendelee kujiingiza kwenye makundi yatakayokuwapo wakati wa kampeni baada ya kushindwa kutochaguliwa kwenye nafasi walizogombea badala yake wakubali maamuzi ya chama.

"Isije ikafika tunapata mtu kwenye mchakato wa chama baada ya kuteuliwa mgombea mmoja, mtu mwingine anachukia na kukihama Chama Cha Mapinduzi na kuhamia vyama vingine vya upinzani, hilo jambo halitegemewi," alifafanua.

Alisema baada ya kutangazwa kwa matokeo ya wagombea wa chama hicho kila mmoja hanabudi kukubaliana na matokeo.

Akitangaza kuihama CHADEMA na kujiunga na CCM, Kiranga alidai alifanya hivyo ili kuhakikisha anashirikiana na wengine kulisukuma gurudumu la maendeleo.

Katibu wa CCM Wilaya ya Singida Mjini, Hamisi Shabani, alisema ratiba ya uchaguzi itakapotangazwa, wanachama wa chama hicho hawanabudi kufanya mchakato wa kistaarabu unaozingatia kanuni na katiba ili kuwapata wanachama wazuri watakaoweza kuwaletea maendeleo wananchi.

# Mashahidi 28 kusikilizwa kesi ya mauaji

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam inatarajia kuanza kusikiliza mashahidi 28 wa Jamhuri katika kesi ya mauaji ya kukusudia dhidi ya Hamis Luwongo, anayedaiwa kumuua mke wake kwa kumchoma moto kwa magunia mawili ya mkaa.

Hatua hiyo imefikiwa jana baada ya upande wa Jamhuri kumsomea mshtakiwa maelezo ya mashahidi na vielelezo sita katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabati.

Pamoja na mashahidi hao, upande wa Jamhuri unatarajia kuwasilisha vielelezo sita ikiwamo ramani ya tukio la mauaji, maelezo ya onyo ya mshtakiwa, ungamo la mshtakiwa kwa mlinzi wa amani, hati ya kumiliki mali na ripoti ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Hata hivyo, mahakama ilimuhoji mshtakiwa kama atakuwa na utetezi pamoja na mashahidi wa kupeleka mahakamani, Luwongo alidai atajitetea mwenyewe na kwamba hatakuwa na shahidi.

Luwongo alidai angeweza kuwaleta ndugu zake na wa upande wa marehemu mke wake kuelezea tatizo lililotokea, lakini atasimama mwenyewe.

Pia alidai ana makovu yaliyosababishwa na kuchomwa visu kutokana na ugomvi wa mara kwa mara kati yake na marehemu mkewe, lakini hawezi kuyatoa kama kielelezo.

"Jalada hili sasa linahamishiwa Mahakama Kuu, hivyo utakuwa mahabusu kusubiri vikao vya kusikiliza kesi yako vitakapopangwa na Msajili wa Mahakama na utapewa nakala ya jalada la mwenendo wa kesi hii kuanzia ulivyopandishwa kizimbani Julai 30, 2019," alisema Hakimu Kabati.

Hata hivyo, mshtakiwa huyo alidai kuwa awali alimwandikia barua Mfawidhi wa Mahakama hiyo kuhusu ndugu wa upande wa mke wake kumkataza mtoto wake kwenda kwa ndugu zake ili waweze kumsomesha kwa kuwa mali na fedha zipo zitazosaidia kulipa ada yake ya shule.

"Mtoto wangu anaishi na ndugu wa mke wangu ninaomba mtoto wangu nimuhudumie, lakini kinachojitokeza hawa ndugu wanampa maneno mwanangu kusudi anichukie," alidai Luwongo.

Katika kesi ya msingi, namba 4 / 2019, mshtakiwa Luwongo Mkazi wa Kigamboni, jijini Dar es Salaam anadaiwa Mei 15, mwaka jana akiwa eneo la Gezaulole Kigamboni kwa makusudi alimuua Naomi Marijani.

# Wakazi Dar waiangukia serikali mgogoro wa ardhi

**Na Maulid Mmbaga**

WAKAZI wa Viwege Kata ya Majohe, wilayani Ilala jijini Dar es Salaam, wameiomba serikali kuingilia kati na kusaidia upatikanaji wa suluhisho la mgogoro wa ardhi baina ya wananchi 59 na mtu anayedaiwa kumiliki eneo hilo.

Wamedai mtu huyo anataka kulipwa fidia ya eneo hilo ambalo wananchi waliuziwa na kujenga makazi kwa muda mrefu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa kikao cha pamoja baina ya wananchi, mmiliki na maofisa wa ardhi wa Manispaa ya Ilala, mmoja wa walalamikaji, Danford Kitwana, alisema alinunua kiwanja katika eneo hilo mwaka 2008 na alifuata taratibu zote za ununuzi wa ardhi.

Alisema ilipofika mwaka 2019 waliletewa taarifa na Mwenyekiti wa Serikali za Mtaa, Amina Kapundi, kuwa eneo waliloweka makazi ni mali ya Wolter Mchome na kudai kuwa mahakama imetoa hukumu ya kuwataka wamlipe fidia kutokana na kuvamia eneo lisilo la kwao.

Aliongeza kuwa walishangazwa na hukumu hiyo kuwa imetokaje wakati kesi bado inaendelea mahakamani, na inaonyesha kuwa aliwashtaki watu 11 na waliweka msimamo kuwa hawawezi kuruhusu eneo kupimwa kwa ajili ya malipo ya fidia mpaka watakapo jiridhisha kuwa kweli ardhi hiyo ni ya Mchome.

Katibu wa walalamikaji, Gausen Msonda, alisema shauri namba 87, la Masonda na wenzake 56 kati ya Mchome na wenzake 11, Februari 20, mwaka huu, Mahakama ya Ardhi wilayani hapo, iliamua kuwa wananchi wanaoishi Viwege shina namba 15 siyo washtakiwa wa Mchome.

"Mchome aje na wenzake 11 aliowashtaki ili wamwonyeshe eneo lake, wananchi kwa pamoja hatuko tayari kuzungumza na mtu tusiye mfahamu hivyo ajitambulishe kwa kuonyesha stakabadhi za umiliki kwa wakazi wa shina namba 15," alisema Msokwa.

Wolter Mchome alisema, eneo hilo alilinunua mwaka 2003 chini ya mjumbe aliyemtambulisha kwa jina moja Daudi, na mwaka 2009 kuna watu 11 walivamia sehemu hiyo na kuanzisha kilimo cha matunda na mboga.

Alisema aliwashtaki na polisi walipofika eneo husika wavamizi walikimbia na baada ya muda kesi ikiwa inaendelea walionekana kurudi na kuendeleza shughuli zao na mahakama iliwazuia na kwamba hadi sasa wananchi wengi wameweka makazi yao.

"Mahakama ilithibitisha kuwa eneo ni langu na mwaka juzi hukumu ilitoka na wale wote waliojenga katika ardhi yangu sitaki kuwavunjia nyumba zao ila wanilipe fidia, nilifungua kesi ndogo ya kukazia hukumu na nikafika kwa mwenyekiti wa serikali ya mtaa kwa ajili ya kumpatia vielelezo vyenye uthibitisho wa mahakama," alisema Mchome.

Mwenyekiti wa eneo hilo, Amina Kapundi alisema eneo hilo lilikuwa na mgogoro kwa kipindi kirefu dhidi ya mmiliki na wananchi wanaotajwa kuvamia na Juni 5, mwaka huu, alipokea barua kutoka kwa ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala iliyomtaka kufanya utambuzi wa ardhi ya mchome.

Alisema alisambaza taarifa hiyo kwa wananchi ili kutambua kinachoendelea katika eneo hilo na huo ni mwendelezo wa hukumu iliyotoka mwaka 2019 na aliongea na wakazi hao zaidi ya mara tatu, kuna waliokubali kulipa fidia, lakini wengine walijitokeza na kupinga hukumu hiyo.

Ofisa ardhi wilayani hapo, Burton Rutta, alisema alipokea taarifa kutoka kwa ofisi ya mkuu wa wilaya na katika kuifanyia kazi, Mchome alifika ofisini na kueleza kwamba kesi iliyokuwa ipo mahakamani imeisha.

Alisema alithibitishiwa na wasaidizi wa DC kwamba kesi hiyo imefika mwisho na ikapelekea kuandika barua kwa wananchi waliopo katika eneo la Mchome.

Aliongeza kuwa hafahamu kuwa eneo hilo lina mgogoro na kuwa kuna kesi, na alimtaka Mchome kumkabidhi hukumu ya mahakama ili aisome ili ajiridhishe kabla ya utekelezaji.




Mratibu wa Shirika linalotetea Haki za Wazee la Tawlae Mkoa wa Shinyanga, Eliasenya Nnko, akitoa elimu ya kupinga ukatili dhidi ya wazee, katika maadhimisho ya Siku ya Kupinga Ukatili wa Wazee Duniani yaliyofanyika kiwilaya katika Kata ya Mwamala, wilayani Shinyanga juzi. **PICHA: MARCO MADUHU.**

# Vitambulisho machinga zaidi 70,000 vyatolewa

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MKOA wa Mwanza umetoa vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo (Machinga) na watoa huduma wadogo 73,000 kwa awamu ya pili mwaka huu, kwa wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri na wilaya zote.

Awamu ya kwanza walikabidhiwa vitambulisho 15,000 vyenye thamani ya Sh. milioni 300 na vilivyogawiwa ni 7,792 huku vitambulisho 7,208 vikiendelea kugawiwa na Sh. 155,840,000 zikiwasilishwa TRA.

Akizungumza wakati akiwakabidhi vitambulisho hivyo, kutoka Ofisi ya Rais Tamisemi vilivyopitia TRA, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, aliwataka viongozi hao kuhakikisha fedha zote zinakwenda benki.

Alisema jumla ya vitambulisho vilivyopokewa Mkoa wa Mwanza ni 88,000 vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.76, hivyo hadi sasa kwa awamu ya kwanza wameuza kwa asilimia 54 na amewataka kuhakikisha wanafunga ndani ya wiki moja pia waratibu wawe makini kwa sababu mfumo umeboreshwa na unafanyakazi ipasavyo hivyo kula hela ya serikali haiwezekani.

"Vitambulisho ni jambo nyeti sana, hivyo tulitilie mkazo vinaweza kukupoteza mweleko kwa ushauri wangu vitambulisho hivi tulivyowagawia awamu ya pili tuvimalize mwezi wa nane," alisema Mongella.

Kwa upande wake Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Emmanuel Tutuba, alisema vitambulisho hivyo vya awamu ya pili wamevipokea kutoka kwa Kaimu Meneja wa TRA, Mkoa wa Mwanza vimegawiwa katika halmashauri nane na wilaya saba za mkoa huo ikiwamo Halmashauri ya Jiji la Mwanza wamepokea vitambulisho 20,000, Ilemela (18,000), Sengerema (6,000), Buchosa (6,000), Ukerewe (5,000), Kwimba (6,000), Misungwi (6,000) na Magu (6,000).

Naye Kaimu Meneja wa TRA Mkoa wa Mwanza, Hoseya Kidasi, alisema wamekabidhi vitambulisho 73,000 na kuunga mkono hatua zinazochukuliwa na mkoa na kuahidi kutatua changamoto ya mtandao ili kusiwe na kikwazo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Kiomoni Kibamba, alisema changamoto waliyokutana nayo ni wakati wakifanya ukaguzi wa vitambulisho kwa wafanyabiashara hao na kukuta wamachinga wa eneo moja ambao wana vitambulisho kwenda eneo jingine na kushauri awamu nyingine vitambulisho hivyo viwekwe picha ya walengwa ili kuondoa changamoto hiyo.

## Mbinga yapata gari la wagonjwa

**Na Gideon Mwakanosya**

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, amekabidhi gari la kisasa la kubebea wagonjwa (Ambulance) kwa ya Kituo cha Afya Mapera Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, ambalo limenunuliwa kwa zaidi ya shilingi milioni 138.

Akitoa taarifa kabla ya uzinduzi na makabidhiano ya gari hilo kwenye ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma mjini Songea, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Juma Mnwele, alisema wamefanikiwa kununua gari hilo kwa kutumia fedha za mapato ya ndani.

Alisema gari hilo la wagonjwa limekatiwa bima kubwa ya Sh. milioni 6.3, na kwamba limepangiwa kutoa huduma za rufani kwa wanawake, watoto na wagonjwa wengine katika Kituo cha Afya Mapera ambacho kimejengwa kwa fedha za serikali shilingi milioni 400.

"Sisi watendaji wa halmashauri tunaona fahari na faraja kuungana na Rais John Magufuli ambaye alituletea milioni 400 za kujenga Kituo cha Afya Mapera na halmashauri tumenunua gari la wagonjwa, yawezekana haijawahi kufanyika mahala pengine," alisema Mnwele.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, aliipongeza Halmashauri ya Mbinga kwa kununua gari la wagonjwa kwa kutumia fedha za mapato ya ndani.

## DC awapa angalizo wanaokwamisha biashara utalii

**Na Restuta Damian,** KYERWA

MKUU wa Wilaya ya Kyerwa mkoani Kagera, Rashid Mwaimu, amesema atachukua hatua za kisheria kwa wananchi ambao wataweka pingamizi kwa utashi wao wenye kupinga maendeleo ya biashara ya utalii yanayovuruga na kusababisha kutofanyika.

Alitoa kauli hiyo mbele ya madiwani wa halmashauri ya wilaya hiyo wakati wakijadili taarifa ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyofanyika kwa kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2019/20 inayolenga kunufaisha wananchi.

Mwaimu alisema kuwa haki itatendeka kwa wakazi wanaostahili kupatiwa fidia ya maeneo yao yaliyochukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa ndege ambao awali ulikuwa ukitumika kutafiti madini.

"Ole wale ambao wanaingia leo kwa kujipenyeza kwenye eneo la uwanja unaotegemewa na Pori la Akiba la Ibanda Kyerwa wilayani Kyerwa na Hifadhi ya Taifa ya Rumanyika wilayani Karagwe ambao utatumika kwa shughuli zao za kitalii," alisema Mwaimu.

## HABARI KITAIFA

# Mbaroni madai kukeketa watoto

**Na Sabato Kasika**

JESHI la Polisi mkoani Mara, limemtia mbaroni mkazi wa kijiji cha Kitarungu, wilayani Serengeti mkoani humo, Mary Onyango (50), kwa tuhuma za kukeketa watoto na wasichana.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Daniel Shillah, alisema, mtuhumiwa huyo alikamatwa na askari polisi kutoka Serengeti Juni 12, mwaka huu eneo la Sirari wilayani Tarime.

Alisema mtuhumiwa huyo alisafirishwa hadi kituo cha Polisi Mugumu kwa ajili ya kuhojiwa kisha kumfikisha kwenye vyombo vya sheria.

"Mtuhumiwa huyo adaiwa kukeketa watoto 10 akishirikiana na wazazi wao kisha kukimbilia Kenya kujificha," alisema Kamanda Shillah.

Alifafanua mtuhumiwa huyo amekuwa akifanya vitendo hivyo na kukimbilia Kenya na kwamba, polisi waliweka mtego na kumnasa Sirari akiwa anatokea nchini humo kununua mahitaji.

"Kwa sasa kuna kesi tatu mahakamani ambazo zinamhusu na baadhi ya wazazi ambao walikamatwa kuhusiana na kitendo hicho kisichofaa kwa mujibu wa sheria za nchi," alisema.

# Wataalamu wahimiza matumizi mbegu bora

**Na Ashton Balaigwa, MIROGORO**

WATAALAMU wa kilimo katika mikoa ya Kanda ya Mashariki wamewataka wakulima kuchukua tahadhari juu ya mabadiliko ya tabianchi, kutokana na mvua za msimu wa kilimo kukatika mapema kuanza kutumia mbegu bora zinazostahimili ukame na visumbufu vya mimea.

Tahadhari hiyo ilitolewa na jopo la watafiti kutoka Taasisi ya Kilimo Tanzania (TARI) wa vituo vya Kanda ya Mashariki waliokutana mkoani Morogoro kwa ajili ya maandalizi ya maonyesho ya kilimo ya Nanenane na namna bora ya kuwasaidia wakulima kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Mratibu wa Utafiti Kanda ya Mashariki kutoka Tari Ilonga, Meshack Makenge, alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi, Tari imezalisha mbegu za mazao ya teknolojia ya kisasa ambazo zinahimili ukame pamoja na changamoto za wadudu.

Mtafiti na mgunduzi wa mbegu za mpunga, Dk. Theodol Kessy wa kituo cha utafiti wa mbegu za mpunga Ifakara wilayani Kilombero, alisema wameshagundua aina mpya za mbegu ambazo zinaweza kulimwa na wakulima katika maeneo ya mabonde na kwenye milima hasa sehemu zenye ukame.

Alisema mbegu hizo zimefanyiwa utafiti katika maeneo mbalimbali na kuonyesha mafanikio, hivyo aliwataka wakulima kuchangamkia mbegu hizo.

Mtafiti usambazaji wa teknolojia zinazozalishwa na Tari Ilonga, Magreth Mchomvu, aliwataka wakulima wanaosumbuliwa na wadudu waharibifu kujitokeza kupata majawabu ya kukomesha wadudu hao, na kujionea teknolojia mpya za mbegu zilizofanyiwa utafiti wa kina.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa daraja la Mto Msingi, lililokuwa limeharibika kwa kipindi kirefu na hivyo kusababisha wananchi kukosa huduma za kijamii kwenye maeneo zinakopatikana huduma hizo, wilayani Mkalama, mkoani Singida. **PICHA: JUMBE ISMAILLY**.

# DC aagiza uchunguzi utata soko

**Na Ashton Balaigwa,** BAGAMOYO

MKUU wa Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani, Zainab Kawawa, ameagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), wilayani humo kuchunguza mchakato wa ujenzi wa soko la nafaka la Magomeni linalodaiwa kugharimu zaidi ya Sh. milioni 600.

Alisema soko hilo limekamilika ujenzi tangu mwaka 2016, lakini halijaanza kutumika.

Alitoa agizo hilo alipokuwa akizungumza katika mkutano wa kusikiliza kero na malalamiko ya wananchi uliofanyika kata ya Magomeni baada ya kupokea malalamiko ya wananchi waliotaka kajua hatima ya soko hilo.

"Serikali inatumia fedha nyingi, Sh. milioni 600 zimeenda hapa, na mimi najiuliza kweli hivi hili soko limejengwa kwa Sh. milioni 600, hili halikubaliki Takukuru lazima waje tujiridhishe, hatuwezi kupoteza fedha ya serikali kiasi hicho," alisema.

Aliagiza uongozi wa Halmashauri ya Bagamoyo kuandaa mpango mkakati kuhakikisha soko hilo linaanza kutumika haraka, kwa manufaa ya wananchi na serikali wakati Takukuru wakiendelea na uchunguzi wao.

Awali, katika kikao hicho baadhi ya wananchi wakiwamo wafanyabiashara walimweleza mkuu wa wilaya kuwa, hawakushirikishwa wakati wa kuibua mradi huo kwa kuwa pamoja na uhitaji wa soko, vipo vipaumbele vingine vya kutekeleza hasa katika kata na kutaka kujua ni lini litatumika ili halmashauri nayo ikusanye kodi.

Diwani wa Kata ya Magomeni, Mwanaharusi Hamisi, alisema yeye kiongozi wa wananchi ameshalilalamikia suala hilo kwenye vikao vya Baraza la Madiwani lakini bado wataalamu wameshindwa kulipatia ufumbuzi na kumwomba mkuu huyo wa wilaya kuingilia kati ili kupata muafaka.

"Mkuu wa wilaya watumishi wanatuangusha, imefikia wakati hata wananchi hawanielewi, kitendo cha zaidi ya Sh. milioni 600 kutumika kwenye mradi mmoja na bado hauleti matokeo, mimi inaniwia ugumu kueleweka kwa wananchi naomba suala hili lichunguzwe," alisema.

Ofisa Biashara halmashauri hiyo, Magdalena Kitilla, alisema kinacho kwamisha soko hilo kufanyakazi ni wafanyabiashara kukimbilia maeneo mengine na mpango wao ni kusimamia sheria walizo jiwekea ikiwamo kuweka makatazo wafanyabiashara kutumia maeneo mengine nje na soko hilo.

# Walalamikia kero umeme muda mrefu

**Na Beatrice Philemon**

WAKAZI 400,000 wa Mtaa wa Mkera, Mvuti Wilaya ya Ilala mkoani Dar es Salaam, wameiomba serikali iwasaidie kuunganishiwa umeme kutokana na kuomba huduma hiyo muda mrefu bila kufungiwa.

Wamesema kuwa wanapata shida kutokana na kuishi gizani, hivyo kushindwa kufanya shughuli za maendeleo.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mkera Mvuti, Cyprian Lihewe, alisema hadi sasa asilimia 90 ya wakazi wa eneo hili wanatumia vibatari, chemli, mishumaa na sola kwa watu wenye kipato cha juu ili kupata mwanga kwenye makazi yao.

"Kutokana na ukosefu wa umeme, kila siku wananchi wanakuja ofisi yetu ya serikali ya mtaa kuuliza umeme utapatikana lini, na sisi kama viongozi tunashindwa kuwapa jibu kwa sababu hatujui umeme utaletwa lini katika eneo hili, ingawa maombi mengi ya kupatiwa umeme yameshapelekwa katika ofisi za Tanesco Kisarawe," alisema.

Alisema baadhi ya wananchi wanasema walipeleka maombi ya kupata umeme kati ya mwaka 2014 na 2019, lakini hawajapata nishati hiyo.

Alieleza kuwa vile vile kuna baadhi ya maeneo nguzo za umeme zimesimikwa katika maeneo yao toka mwaka 2014, lakini hadi leo hazina nyaya za umeme, na zinaendelea kuoza.

"Kutokana na ukosefu wa umeme, maendeleo mengi yamesimama katika mtaa wa Mkera Mvuti, wananchi wanashindwa kuanzisha miradi ya maendeleo," alisema.

Alisema ingawa Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alipotembelea Mtaa wa Kitonga Desemba 2019 kuzungumza na wananchi, kujua changamoto zao na baadaye kuwaahidi kuwa hadi kufikia Mei mwaka huu, wananchi watakuwa wamepata umeme, hadi sasa asilimia 90 ya wananchi katika mtaa wake hawajapata umeme.

Meneja wa Tanesco- Kisarawe, Mhandisi Nyanda Busumabu, aliwaomba wananchi wawe wavumilivu na wastahimilivu watapata umeme.

"Hadi kufikia mwisho wa mwezi Septemba wananchi watapata umeme kwa sababu serikali kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA) mwaka jana ilizindua mradi mpya wa kusambaza umeme kwenye vijiji na mitaa vilivyopo pembezoni mwa miji na majiji unaojulikana kama ' Peri-Urban electrification," alisema.

Alisema huu ni mradi wa miezi tisa ambao unatekelezwa na REA katika maeneo ya Mbondole, Kitonga, Kidole, Mvuti na Uwanja wa Nyani.

"Wananchi wa Mtaa wa Mkera wapo ndani ya kitongoji cha Mvuti, ambapo katika kata ya Msongola kuna maeneo mengine ambayo yatapata umeme," alisema.

Mwamko mpya haki za weusi Floyd alipouawa

Ukurasa 13






Ukurasa 12

**Ni kiama mamluki kura za maoni CCM...**

siasa
JUMATANO JUNI 17, 2020
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

# Mifumo, miongozo, taratibu vitanzi vinavyokwamisha kufikiwa 50/50

**Na Mary Geofrey**

IKIWA imesalia miezi minne kufanyika uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani upungufu wa kisheria, mifumo na taratibu zinazowakwamisha wanawake kushiriki na kuchaguliwa kuwa viongozi wa kisiasa yameibuliwa.

Mtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi kwa kushirikiana na Mfuko wa Udhamini wa Wanawake Tanzania (WFT) wanafanya uchambuzi wa sheria tano za uchaguzi kwa mrengo wa jinsia ili kuangalia vikwazo vinavyowazuia kinamama kushiriki kikamilifu.

Uchambuzi wao ulilenga kuibua mambo yaliyojitokeza kwenye baadhi ya Sheria za Uchaguzi ili kubainisha vikwazo katika kutekeleza azma ya ujenzi wa demokrasia shirikishi kwa mrengo wa jinsia.

Mwenyekiti wa WFT, Prof. Ruth Meena, akitoa mrejesho anawaeleza wanahabari katika mkutano wa kimtandao, kuwa katika sheria walizozifanyia uchambuzi wamebaini mapengo kadhaa.

Anasema: "Lengo ni kutoa mapendekezo mahususi yatakayoongoza wadau mbalimbali katika kuchukua hatua kukabiliana na sheria za ubaguzi wa aina zote hususani ubaguzi wa jinsia kwenye mchakato wa uchaguzi."

Pamoja na sheria hizo, walifanya uchambuzi wa Katiba za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na ile ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zikiwa sheria mama zinazoongoza utunzi wa sheria zote za nchini, anaongeza.

Aidha, waliangazia mfumo wa uchaguzi, haki ya kupiga kura, ya kuteuliwa na uwazi kwenye uteuzi.

Anasema walizichunguza pia gharama za uchaguzi, uwajibikaji na wajibu wa vyombo vya habari katika uchaguzi mkuu na kudadavua kasoro zake ambazo ni kikwazo kwa mwanamke kushiriki uchaguzi.




Profesa Ruth Meena, mwana zuoni wa sayansi ya siasa akitoa nasaha zake. **PICHA MTANDAO.**

### SHERIA ZILIZOPITIWA

Anataja sheria walizofanyia uchambuzi kuwa ni Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 ya mwaka 2015 na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar namba 4 mwaka 2018.

Nyingine ni ile ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa namba 4 ya mwaka 1979 namba 292 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2010 na mwaka 2015, Sheria ya Serikali za Mitaa inayofahamika kama Mamlaka za Wilaya Sura 287 na Sheria za Serikali za Mitaa za Mamlaka za Miji sura ya 288 na Mamlaka za Wilaya sura ya 287.

"Katika uchambuzi tuliofanya katika maeneo yote hayo tumebaini kuwapo kwa upungufu wa sheria na miongozo inayowafanya wanawake kushindwa kushiriki kikamilifu katika uchaguzi na tayari tumewasilisha taarifa hii kwa vyombo vyenye mamlaka kama Bunge kwa ajili ya kufanya marekebisho," anasema.

### MFUMO WA UCHAGUZI

Profesa Meena anasema mfumo wa uchaguzi unaongozwa na dhana ya kuwa ushindi anapata yeyote bila kujali uwakilishi na hauko rafiki kwenye uwakilishi wa makundi yote na demokrasia shirikishi.

Anasema takwimu za nchi nyingi duniani zinazotumia mfumo huo zinaonyesha kwamba ufikiaji wa azma ya usawa wa jinsia ni mgumu.

### HAKI KUPIGA KURA

Mwenyekiti wa TWF anasema katiba zote mbili ya Tanzania Bara na Visiwani zinabainisha haki sawa ya kupiga kura kwa raia wote waliotimiza miaka 18 na kuendelea.

"Kwa mfano, takribani asilimia 95 ya wapigakura waliojiandikisha kwa mwaka 2015 walipiga kura wanawake wakiwa asilimia 53 ya wapigakura wote kwa mwaka huo kwa mujibu wa takwimu za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) za mwaka 2016," anasema Prof. Meena.

Anaeleza zaidi kuwa kulikuwapo na ongezeko la wanawake waliojiandikisha kupiga kura kwenye uchaguzi wa mwaka 2015 kwa asilimia 4.4 ya wale waliojiandikisha katika uchaguzi wa 2010.

### HAKI KUTEULIWA

Anasema uteuzi wa wagombea ni msingi wa kupata wagombea wenye sifa na hatimaye viongozi bora.

Upungufu uliopo ni kuwa wagombea wote, kwenye mchakato wa uchaguzi, lazima wawe ni wanachama wa vyama vya siasa na waliopendekezwa na vyama husika.

Anataja vifungu vinavyowabana ni 26 (2) (d) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 2018 na kifungu cha 36 cha Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977.

Anasema kwenye muktadha unaoongozwa na mfumo dume ndani ya vyama vya siasa na uongozi usiyo na utashi wa kuzingatia usawa wa jinsia, sharti hili huwaumiza wanawake zaidi.

"Takwimu za uchaguzi zote zinaonyesha jinsi vyama vinavyobagua wanawake kwenye uteuzi," anaeleza Prof. Meena.

Anatolea mfano mwaka 2015 asilimia ya wagombea viti vya ubunge upande wa wanawake ilikuwa: ACT- Wazalendo asilimia 15, CUF asilimia 11, CCM asilimia 9 na Chama cha Demokrasia na Maendeleo asilimia 6.

"Hali hii inaonyesha kutokuwapo na utashi wa siasa wa kutekeleza azma ya ujenzi wa

INAENDELEA UK.12

# Ni kiama mamluki kura za maoni CCM...

• Polepole: Udhibiti kielektroniki unawasubiri

**Na Sabato Kasika**

MOJA ya mambo yaliyokuwa yakiibua malalamiko miongoni mwa makada wa CCM katika mchakato wa kura za maoni kupata wagombea wa kukiwakilisha chama hicho katika uchaguzi ni madai ya kuwapo mamluki.

Katika mchakato huo, walikuwa wakidai kuwapo 'walaghai' waliokuwa wakichukuliwa na baadhi ya wagombea na kupiga kura za maoni ili kuwasaidia kushinda.

Hali hiyo ilisababisha malalamiko ndani ya chama hicho kwa vile ilidaiwa kuwa hata kitabu chenye majina ya wanachama hakikutumika ipasavyo lengo ni kumbeba mgombea anayetakiwa na baadhi ya vigogo.

Kuna wakati ilidaiwa kwenye vyombo vya habari kuwa kadi za CCM zilikuwa zikitupwa mitaani au kuchanwa na mamluki baada ya kumaliza mchakato wa kura maoni.

Lakini sasa CCM mpya imekuja na utaratibu ambao utawaweka nje wale waliokuwa wamezoa kufanya mchezo huo wa kununua kadi na kugawa kwa mamluki, ili wawasaidie kupata ushindi katika kura za maoni.

CCM inajinasibu kuwa imesimama ipasavyo, kusimamia, haki na mchakato wa maadili ili kupata wanachama bora kwa ajili ya kukifanya chama hicho kuendelea kuwa na umoja na mshikamano.

Kwa maana hiyo, ni wazi kwamba waliozoea ujanja na wizi safari hii watakwama, hasa kutokana na maelezo kwamba chama hicho kimekuwa kikiwaonya mara kwa mara na sasa kimetangaza utaratibu mpya wa kupata wagombea wa ubunge na udiwani kwa misingi na taratibu tofauti na ile iliyokuwa inapindisha sheria.



Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole, akitangaza vita na mamluki wa kura za maoni. **PICHA: MTANDAO.**

### MKAKATI MPYA

Akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam hivi karibuni, Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM Taifa, Humphrey Polepole, anasema utaratibu wa kupata wagombea umebadilika na sasa ni matumizi ya teknolojia.

Anasema kadi na vitambulisho vyote vitakuwa katika mfumo wa kielektroniki kwa lengo la kuepuka mamluki wa vikao vya chama hicho, katika kuwapata makada wagombea kwenye uchaguzi ujao.

"Kipindi hiki tumeweka utaratibu wa kielektroniki na vitambulisho janja havitakuwa na nafasi. Mjumbe atatoa kitambulisho na kutakuwa na utambuzi kielektroniki hali itakayodhibiti mamluki. Tunataka haki itamalaki," anasema Polepole.

Anaelekeza kuwa chama baada ya kutafakari kimekuja na utaratibu uliowekwa kwenye katiba na kanuni ya uchaguzi na utatumika kipindi hiki cha uchaguzi mkuu ili kujadili na kupendekeza wagombea wanaostahili.

"Huo ndiyo utaratibu mpya ambao chama kitautumia kupata wagombea ubunge na uwakilishi katika uchaguzi mkuu, baada ya kubaini kuwa uliotumika mwaka 2015 ulikuwa na upungufu," anasema Polepole.

Anaeleza kuwa mchakato uliotumika mwaka huo wa uchaguzi uliacha mianya ya rushwa na uvunjifu wa taratibu na hawataki hali hiyo ijirudie tena na kuanzia mwaka huu wa 2020 utaratibu mpya utatumiwa.

Anasema, chama hicho kinawafahamu watoa mlungula majimboni kwa majina na fedha wanazotoa na kwamba kitawakataa, kwa vile rushwa ni adui wa haki, tena haikubaliki na haina nafasi kwenye chama hicho.

"Niwaambie kuwa tunafuatilia kwa karibu sana sarakasi, vurumai na figisu, ambazo watu wanaotafuta uongozi kwa hila wanaendelea nazo katika maeneo kadhaa nchini," anawaonya.

Kiongozi huyo anasema, chama kinawafahamu kwa majina wote wanaotoa fedha ili kuhonga wajumbe wa vikao na kwamba uongozi wa awamu ya tano umejipanga kuzuia rushwa, kwa vile kufanya hivyo ni kumuudhi hata Mungu.

"Niseme wala rushwa hawana nafasi kwenye hiki chama, hivyo watu watende haki na kuwa waaminifu kwa Chama Cha Mapinduzi ili kiendelee kutimiza wajibu wake kwa Watanzania," anasema.

### HAKUNA MBWEMBWE

Kwa utaratibu wa sasa, Polepole anasema, kada wa CCM anayetaka kuwania uongozi, ni marufuku kwenda kuchukua fomu kwa mbwembwe, bali aifuate kimya kimya na kurudi nyumbani kuijaza kisha kuirejesha.

"Utaratibu wa sasa utahusisha Kamati ya Siasa ya Wilaya, Kamati ya Siasa ya Mkoa na Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa kwa ajili ya kuwajadili waliochukua fomu na kutoa mapendekezo," anasema.

Anafafanua kuwa Kamati Kuu itateua majina matatu yatakayopelekwa kwenye Mkutano Mkuu wa Jimbo na kwamba majina hayo yatakuwa ni siri na yatawekwa muhuri wa moto.

Anaongeza kwamba, baada ya hapo yatarejeshwa katika mkutano wa jimbo wenye wajumbe kati ya 800 hadi 1,000 ambao utakuwa na jukumu la kuyapigia kura na kutengenezewa muhtasari utakaoonyesha kila mgombea na kura zake.

"Baada ya hapo majina hayo yatarudishwa kwa wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (Nec), lakini jambo la msingi, mwanachama anayetaka kugombea haruhusiwi kuchukua fomu kwa mbwembwe," anasema.

### BUNGE KUVUNJWA

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Watanzania lilivunjwa jana na Rais John Magufuli, hivyo wabunge wanarudi majimboni kwa ajili ya mchakato wa kutetea nafasi hiyo kwa lengo la kurejea tena bungeni baada ya uchaguzi mkuu.

Wapo baadhi ya wabunge, ambao wametangaza kupumzika siasa akiwamo Mbunge wa Muleba Kusini mkoani Kagera, Prof. Anna Tibaijuka (CCM), ambaye anasema, miaka 10 aliyoongoza jimbo hilo inatosha.

Aidha, baadhi ya wabunge wanatarajia kukutana na upinzani majimboni mwao, kutokana na ukweli kwamba kila mwaka wa uchaguzi, ndani ya vyama huwa kuna mchuano mkali kupata mwakilishi mmoja wa chama.

---

## MIFUMO, MIONGOZO, TARATIBU VITANZI VINAVYOKWAMISHA KUFIKIWA 50/50

**INATOKA UK.11**

demokrasia shirikishi kwa mrengo wa jinsia," anasema Prof. Meena.

### UWAZI UTEUZI

Profesa Meena anasema taratibu za uteuzi ndani ya vyama haziko wazi, kwenye mfumo wa uteuzi, hasa kwenye kuzingatia msingi wa usawa wa kijinsia.

Anafafanua kuwa, sheria ziko kimya kwenye kuwajibisha vyama vinavyokiuka sharti la usawa wa jinsia katika uteuzi wa wanawake kugombea nafasi mbalimbali za uchaguzi.

### GHARAMA ZA UCHAGUZI

Prof. Meena anaeleza kuwa kuhusu gharama za uchaguzi, sheria zinatoa sharti la kuweka dhamana ya kiwango fulani cha pesa kwa wagombea, huku akitolea mfano kiwango cha Sh.1,000,000 kwa urais Bara na Sh. 2,000,000 urais Zanzibar.

"Viwango hivi ni kikwazo cha wanawake wenye uwezo wa uongozi, lakini hawana uwezo wa kifedha. Ni kikwazo cha kutosha kumfanya mwanamke kushindwa kuwania nafasi ya urais," anasisitiza Prof. Meena.

### UWAJIBIKAJI

Katika suala la uwajibikaji, Profesa anasema sheria haijatoa meno kwa NEC kuwajibisha vyama vya siasa, ambavyo kwenye uteuzi, hawazingatii usawa wa jinsia kwenye uteuzi wao.

### VITI MAALUM

Anaeleza kuwa, azma ya kuwapo kwa viti maalum imetumiwa kwa njia iliyoingiza ubaguzi kati ya wajumbe wa kuchaguliwa majimboni na wale wanaoingia bungeni kwa kuteuliwa.

> Viwango hivi ni kikwazo cha wanawake wenye uwezo wa uongozi, lakini hawana uwezo wa kifedha. Ni kikwazo cha kutosha kumfanya mwanamke kushindwa kuwania nafasi ya urais," anasisitiza Prof. Meena.

Anasema mbunge wa viti maalum hawezi kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu, hapewi fedha za jimbo kwa ajili kuwakilisha na hubaguliwa kuingia kwenye kamati mbalimbali za bunge.

"Kuna haja ya kuboresha sheria za viti maalum ambavyo kimsingi hupewa wanawake ambao ndio haswa wapo nyuma katika kuwania nafasi hizi za uongozi kutokana na sheria hizi kandamizi," anasema Prof. Meena.

### VYOMBO VYA HABARI

Mwenyekiti wa huyo wa WFT, Prof. Meena, anasema, lengo la kuwasilisha uchambuzi huo kwa vyombo vya habari ni kuwezesha wanahabari kupata taarifa za kina zilizotokana na uchambuzi wa sheria zilizochambuliwa kwa mrengo wa jinsia.

Anasema wanapaswa kufahamu kwa sababu ni kiungo muhimu kwenye ujenzi wa demokrasia shirikishi na kwenye harakati za ukombozi wa wanawake kimapinduzi.

"Aidha, wanahabari ni kiungo kinachounganisha jamii, wanaowania kuomba dhamana ya uongozi kwa wapiga kura au kuwasilisha madai ya wapiga kura kwa wale wanowania kuomba dhamana ya uongozi," anasema Prof. Meena na kuongeza kuwa,

"Wanahabari wanapaswa kujielimisha kuhusu masuala ya jinsia katika mchakato wote wa uchaguzi ili kubaini mapengo ya utekelezwaji wa sheria za uchaguzi kwa mrengo wa jinsia. Maarifa haya yatawapa wanahabari nyenzo ya kutetea haki ya ushiriki wa wanawake katika mchakato wa uchaguzi."

# Mwamko mpya haki za weusi Floyd alipouawa

**Na Ani Jozeni**

## • Polisi yavunjwa, ajira zake kuanza upya




Mamia ya Wamarekani wakiandamana mitaani na ujumbe unaotaka haki ya kuishi ya watu weusi. **PICHA: MTANDAO.**

JINA George Floyd limeingia katika historia kwa kusababisha kimbunga cha moto Marekani na kwingineko duniani kudai haki, usawa na utu wa mtu mweusi.

Floyd aliuawa kwa kukandamizwa na goti la polisi kooni kwa dakika nane huku akiwa amefungwa mikono baada ya kukamatwa kwa madai ya kutoa noti feki ya dola 20 (takribani Shilingi 46,000.)

Inaelezwa kuwa hakuwa katika hali ya kotoroka au kumdhuru polisi kwa njia yoyote, na polisi aliyemuua alikuwa na wenzake kadhaa ingekuwa ni suala la fujo bado mtu huyo angedhibitiwa.

Ilikuwa kwamba polisi wazungu wamepata nafasi ya kuua mtu mwingine mweusi, wakaitumia.

Baada ya kijana huyo mwenye umri wa miaka 46 kuuawa halafu kilichotokea na kupigwa picha za video zikasambazwa katika mtandao, harakati ya 'Black Lives Matter' (Maisha ya Weusi ni Muhimu) ilishtuka.

Hapakuwa na haja ya kuanzisha maandamano kwa kuwasiliana kwa mfano kama inavyotokea katika maandamano mengine yaliyotangulia, ambayo kimsingi yalikuwa ya vijana wa vyuo na vyuo vikuu, kwani hii ni harakati ya wananchi wa kawaida pamoja na makundi ya vyuo na wafanyakazi.

Yanakuwa na viongozi wa kijumuiya na wapangaji shughuli wanaopatikana papo kwa papo, kwani kila aliyeguswa anatoka kuandamana pia.

Athari muhimu zaidi ya kifo cha kijana huyo ni taifa la Marekani kutambua kuwa kuna walakini mkubwa katika sheria zinazotawala matumizi ya nguvu katika uendeshajii wa kukamata na kuhoji watu unaofanywa na Jeshi la Polisi.

Maeneo mengi nchini Marekani utaratibu wa kubadili kabisa mfumo huo umeanza. Polisi ni eneo mojawapo la mamlaka ya serikali za majimbo na jiji la Minneapolis ambako mauaji dhidi ya mtu mwingine mweusi yamefikia kuvunjwa kwa Idara ya Polisi na kuteuliwa jopo kuiunda upya.

Dhana ya msingi ni kuweka kanuni zinazoeleweka na zitakazofuatwa kung'oa ubaguzi katika utendaji kazi.

Wimbi hilo la kuhoji kuuawa kwa George Floyd halikuwa la amani kama maandamano ya miaka iliyopita yakiongozwa na mpiganaji mwenye nishani ya Nobel, Mchungaji Dk. Martin Luther-King Jr miaka ya 1960 ila ni harakati zinazoendana na Black Panther, kundi la Black Muslims (Waislamu weusi) na wengine.

Hawakujielekeza kwa Uafrika wao ila kudai haki na heshima kwa Mmarekani mweusi kama binadamu au raia mwingine yeyote wa nchi hiyo ila kulikuwa na mapambano na hasira za kuvunja maduka, kuiba vito vya thamani, kuchoma moto vituo vya polisi, na athari nyingine lukuki.

Hata hivyo hawakulenga kuua watu, labda polisi kujeruhiwa magari yao au vituo vyao vikishambuliwa na waandamanaji katika miji tofauti.

> Taarifa zinaeleza kuwa kijana huyo hakuwa na kitambulisho kwa hivyo akakimbia polisi alipowaona wanakaribia, wakamfikia, wakamkamata na kumzuia chini na inaelekea alikabwa au kubanwa mshipa na kufariki, kama ilivyotokea kwa Floyd.

Rais Donald Trump, alijikuta katika wakati mgumu kwani kwa silika zake kisiasa anajua kuwa wahalifu hao ni Wazungu siasa kali, penginepo wanaamini ni Wakristo zaidi yaani wa rangi, kama dini ya Wazungu na wanaopambana nao siyo wanaompigia kura. Anajaribu alivyoweza kupunguza makali ya udhalimu wa polisi kwa kawaida yao, akasisitiza umuhimu wa kutii sheria amani iendelee kutawala kote, akakwama. Inapoonekana kuwa maandamano yanaenea kote nchini Marekani akatoa rai kuwa polisi wa jeshi nao waingie kudhibiti waandamanaji, wakuu wa Wizara ya Ulinzi wakasema hiyo si kazi ya jeshi, ila hatari halisi inayoinyemelea nchi.

Mkuu wa Majeshi Jenerali Mike Muller akaomba radhi kwa kupigwa picha akiwa na Rais Trump, wakati mapambano yanaendelea kote nchini, na jeshi linapinga kuingilia siasa hiyo.

Umuhimu wa maandamano hayo ulidhihirika zaidi pale yalipochipuka katika nchi nyingine kwa vitendo vya ukatili wa polisi vinavyofanana na hivyo vya Minneapolis baada ya wanaharakati wa nchi hizo kuwapiga picha polisi wakifanya ukatili.

Nchini Ufaransa wimbi la maandamano lilianza wakati kijana wa asili ya Kiafrika ambaye aliuawa mwaka 2016 na polisi jijini Paris wakati wa kukaguliwa vitambulisho, na upinzani kuhusu ukatili huo umeendelea tangu wakati huo kwani hatua za wazi dhidi ya polisi waliohusika zilichukuliwa.

Baada ya matukio ya Marekani, ndiyo dunia nzima ikaanza kujua jina la Adama Traore, aliyekuwa na umri wa miaka 24 wakati akiuawa kimakosa.

Taarifa zinaeleza kuwa kijana huyo hakuwa na kitambulisho kwa hivyo akakimbia polisi alipowaona wanakaribia, wakamfikia, wakamkamata na kumzuia chini na inaelekea alikabwa au kubanwa mshipa na kufariki, kama ilivyotokea kwa Floyd.

Taarifa za ziada zinasema kuwa hivi majuzi Idara ya Polisi ilitoa taarifa ya mwisho ya uchunguzi wa suala hilo na kufikia tamati kuwa kifo kilikuwa ni bahati mbaya na polisi waliohusika hawakutenda kosa lolote.

Suala la Floyd lilipozuka, wanaharakati Ufaransa wakakumbushia ya Adama Traore, wakati nchini Canada maandamano yalianza polisi walipopigwa picha wakimpiga na kumtupa chini kiongozi wa kabila la jadi la Wahindi.

Waliotoka barabarani wanasema polisi nchini Canada hawaheshimu kabisa wakazi wa jadi, huwanyang'anya watoto wao wakuzwe katika taasisi za serikali na wanahofia pia kupokonywa ardhi waliyobaki nayo.

Wakati nchini Marekani wafuasi wa Rais Trump na makundi ya wanaharakati wa mrengo wa kulia ambao hawahangaishwi na ubaguzi wa rangi katika mazoea ya polisi wakifanya kazi ndiyo waliandaa makundi ya kufanya maandamano kupinga yale ya wanaotaka mabadiliko, nchini Ufaransa hata polisi wenyewe waliandamana.

Ufaransa ni nchi ambayo hata polisi wana vyama vya wafanyakazi na wanafanya maandamano mara kadhaa walikuwa na utetezi kama huo, na kimsingi ni kutetea taratibu zenye uimla na ubaguzi wanazoona ni muhimu kwa kulinda amani.

Kama ilivyo Marekani, likitokea tatizo la uvujifu wa amani kwa mfano wizi wa kutumia silaha, polisi wanatafuta mtu mweusi au wa asili ya Kiarabu nchini Ufaransa na hawajali kivile kama ni huyu au lah, mradi alikuwa ni wa rangi hiyo. Yote hayo huibua chuki zinazotokana na kuua kwa kusudia, lakini sasa huenda mambo haya yakapungua au kuelekea kuisha.

# Yaliyojiri Bunge la 11



Wabunge wakiwa kazini bungeni kuwatumikia wapigakura na Taifa. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

HAUCHI hauchi kumekucha! Bunge la 11 limemaliza kazi na limevunjwa rasmi na sasa kinachoendelea ni mchakato na mikakati ya wabunge na wagombea kuingia kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2020.

Bunge la 11 lilifanya vikao wakati kukiwa na hofu kubwa ya corona au Covid-19 kwani lilianza kipindi ambacho maradhi hayo yameshika kasi na kusababisha hofu kwa kuwapo mikusanyiko mikubwa kama bunge lenye watu zaidi ya 200 kulionekana kama sehemu hatarishi.

Wapigakura wanapolipa mkono wa kwaheri bunge hili, kuna mengi ya kukumbukwa na mojawapo ni kwamba lilifanyika bila wapigakura kuwasikia na kuwaona wawakilishi wao wakichangia masuala mbalimbali kwani halikuonekana mubashara.

Matangazo mubashara yalikuwa kwenye kipindi cha maswali na majibu na uwasilishaji wa hotuba za bajeti. Hatua hiyo, iliwalazimisha wabunge na washirika wao kurusha michango na hotuba zao kwenye video kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii.

Hata hivyo, si wote walioweza kuona video za kazi zao kwa sababu za kiteknolojia kwani si wote wanaomiliki simujanja hasa wanaoishi vijijini.

Ni wazi kuwa wapigakura hawakusikia wabunge wakizungumzia matatizo yao kama shida ya maji, barabara, huduma za afya, matatizo ya kilimo, ufugaji na migogoro mingine. Hata hivyo kivumbi kinarudi majimboni kuelezana na kukagua kazi za wabunge hao.

> “Ni bunge ambalo wabunge wengine wa upinzani kutoka Chadema, Peter Lijualikali, David Silinde, Anthony Komu, Wilfred Rwakatare na Joseph Selasini walivuliwa uanachama wa chama hicho.

**MASHAMBULIZI**

Aidha, Bunge linapoahirishwa jana kumbukumbu zinaonyesha kuwa lilishuhudia taarifa za mmoja wao Tundu Lissu, akishambuliwa kwa risasi akiwa nyumbani kwake mjini Dodoma mwaka 2017.

Waliomshambulia hawajafahamika na polisi inaendelea na uchunguzi.

Aidha, wiki iliyopita Mwenyekiti wa Chadema na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani bungeni, Freeman Mbowe, alidai kushambuliwa na watu wasiojulikana wakati akirejea nyumbani kwake mjini Dodoma. Hata hivyo, polisi haijathibitisha madai yake na ilieleza kuwa alikuwa ametumia kinywaji.

**TIMUATIMUA WABUNGE**

Mwaka 2017 uliandika historia bungeni kutokana na mgogoro wa viongozi wa CUF, Katibu Mkuu, Seif Shariff Hamad na Mwenyekiti Profesa Ibrahimu Lipumba, kuishia kwa kishindo kilichosababisha kufukuzwa uanachama na kupoteza ubunge wabunge nane wa viti maalumu.

Hatua hiyo ilichukuliwa na Mwenyekiti Lipumba baada ya bunge la bajeti Julai 2017, akitangaza kuwafutia uanachama wabunge viti maalum wanane pamoja na madiwani wawili kwa tuhuma mbalimbali ikiwa ni pamoja na utovu wa nidhamu.

Baada ya kutimuliwa wabunge hao wa viti maalum waliteuliwa wengine kujaza nafasi za wenzao, kuapishwa na kuingia bungeni wakitambulika kama wana CUF watiifu kwa Lipumba, mwenyekiti anayetambuliwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

Ni bunge ambalo wabunge wengine wa upinzani kutoka Chadema, Peter Lijualikali, David Silinde, Anthony Komu, Wilfred Rwakatare na Joseph Selasini walivuliwa uanachama wa chama hicho.

Hatua hiyo ilikuja baada ya kukaidi maelekezo ya chama ya kuwataka kutoshiriki mikutano ya bunge kwa siku 14 ili kujiweka karantini nao walikataa na kuendelea kuhudhuria vikao vya bunge.

**PIGO KWA VYAMA**

Halikadhalika Bunge la 11 lilishuhudia wapinzani wakipata pigo kubwa, baada ya wabunge wa chama kikuu cha upinzani cha Chadema kukimbia chama hicho kwa kuvutiwa na utendaji kazi uliotukuka wa serikali ya Rais John Magufuli. Kuanzia hapo ikawa kawaida kwa CCM kuvuna wanachama wapya kutoka Chadema na CUF.

Wabunge, madiwani na wanachama wengine wa Chadema walikimbilia CCM miongoni mwao ni Mwita Waitara aliyekuwa Ukonga ambaye sasa ni Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ( akiratibu elimu).

Yupo Godwin Moleli Mbunge wa Siha na Naibu wa Waziri wa Afya, aliyeteuliwa kushika nafasi hiyo mwezi uliopita.

Wengine walioiacha Chadema ni Julius Kalanga (Monduli), Chacha Ryoba (Serengeti), James Ole Millya (Simanjiro), Pauline Gekul (Babati Mjini) na Joseph Mkundi (Ukerewe) na sasa Peter Lijuakali (Kilombero), Joseph Silinde (Momba) na Cecil Mwambe (Ndanda).

Kwa upande wa CUF ni Maulid Mtulia (Kinondoni) na Zuberi Kuchauka (Liwale).

**CCM NA OFA ZAKE**

Licha ya Silinde, Mwambe na Lijualikali kutangaza kuwa wanahamia CCM, wanaeleza nia yao wakati huu ikiwa imepita miezi nane baada ya CCM kutoa ofa kwa wabunge wa upinzani kujiunga nayo.

Itakumbukwa CCM haikufanya ajizi, baada ya kuona wimbi la wabunge, madiwani na wanachama wa upinzani wakivutiwa na JPM, Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu Oktoba 30 ilitangaza Novemba 15, 2019 kuwa siku ya mwisho ya kupokea maombi ya wapinzani wenye nia ya kuingia CCM ili kuchaguliwa kugombea nafasi mbalimbali.

**KUPOTEZA UBUNGE**

Wabunge wa upinzani Tundu Lissu Mbunge wa Singida Mashariki na Joshua Nassari walivuliwa ubunge. Aidha, Lazaro Nyalandu, aliacha ubunge na kujiunga na Chadema.

Lissu na Nassari waliondoka kwa sababu za kutoonekana bungeni kwa muda mrefu, lakini bila kuiarifu kimaandishi Ofisi ya Spika.

**WABUNGE KUFUNGWA**

Bunge limeshuhudia wabunge wakitupwa gereza kwa miezi kadhaa nao ni Joseph Mbilinyi ‘Sugu’ wa Mbeya Miji alifungwa jela miezi mitano na Mahakama ya Mbeya kwa kosa la kutumia lugha ya kutusi dhidi ya Rais John Magufuli.

Aidha, Peter Lijualikali wa Kilombero naye alianza kutumia kifungwa miezi sita kabla ya Mahakama Kuu haijafuta adhabu hiyo kutokana na kukosekana ushahidi. Alipatikana na hatia ya kufanya fujo na kuhukumiwa kifungo na Mahakama ya Kilombero.

**KULIKONI VITA MAALUM**

Bunge lililomaliza muda wake jana, liligubikwa na madai ya udhalilishaji wa wabunge wanawake waliofika bungeni kwa utaratibu wa viti maalumu.

Inadaiwa kuwa viti maalum vimetumiwa kuteua wabunge, lakini kwa njia ambazo zinakosolewa na kuhusishwa na unyanyasaji kijinsia na ngono.

Suala hilo kwa miaka mingi limekuwa likijadiliwa kimyakimya, lakini mwaka huu limeibuka bungeni kwa sura mpya ambayo baadhi ya wabunge wanataka viongozi wahusika kwenye uteuzi huo wachunguzwe iwapo wanawanyanyasa kinamama.

Kwenye mitandao ya kijamii kumeibuka mijadala wakikosoa na kutaka eneo bunge hilo lichunguzwe na kuwekwe utaratibu ili kuondoa sintofahamu katika uteuzi.

Wanajamii wanahoji inakuwaje viti maalumu vihusishe marafiki, wakati mwingine wanafamilia na hata watu wenye uhusiano wa unyumba?

Baadhi ya mitandao ikiwamo ya wanahabari wanawake inahoji kwanini wabunge na madiwani wa viti maalumu wasiwajibike kwa wananchi badala yake wawajibike kwa vyama vyao? Wakati wanatakiwa kuwasemea wanawake na watoto na wanyonge ambao hawasikiki wala kuwa na mtetezi.

Katika mijadala hiyo wanasisitiza uwazi, kuboresha sheria ya kuteua wawakilishi hao na kuandaa miongozo na kanuni zinazoeleweka ili kuondokana na sintofahamu iliyomo kwenye eneo hilo la ubunge.





# Mtaalamu afafanua kuhusu tiba shufaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa kuimarishwa kwa huduma mahususi kwa watu wenye magonjwa sugu ambao wameumwa kwa muda mrefu bila kupata uponyaji (tiba shufaa), kutasaidia kupunguza gharama za matibabu hasa kipindi hiki cha ugonjwa wa corona.

Kupitia tiba hiyo, mtoa huduma anapaswa kumtembelea mgonjwa nyumbani kwa ajili ya matibabu ya mara kwa mara na kutoa ushauri kwa wanaomuuguza mgonjwa huyo.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Programu ya Tiba Shufaa inayotolewa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Paul Mmbando, katika kikao cha kuangalia utekelezaji wa mkakati wa kisera wa tiba hiyo kilichowakutanisha wataalamu mbalimbali wa Wizara ya Afya na taasisi nyingine za serikali.

Alisema mkakati huo wa kisera wa tiba shufaa unapaswa kutiliwa mkazo kipindi hichi cha uwepo wa ugonjwa wa corona na huduma hiyo ipatikane kwa ngazi zote ili kuwasaidia wagonjwa sugu.

"Uwapo wa ugonjwa wa corona umebadili maisha yetu kwa ujumla, tofauti na tulivyozoea kwa wagonjwa hawa ambao wengi wao wapo majumbani, ni changamoto katika kuwahudumia ili kuwapunguzia maumivu kama vile wagonjwa wa saratani," alisema.

Alisema hadi sasa Tanzania kuna vituo 65 vinavyotoa huduma ya tiba hiyo ikilinganishwa na awali kulikuwa na vituo vinne.

"Miongoni mwa mafanikio tunayojivunia katika kipindi cha uongozi wa Rais John Magufuli ni kutungwa kwa sera ya tiba hii mwaka 2016 kwa muda mfupi huduma ya tiba shufaa imeimarika," alisema.

Dk. Mmbando alisema ni muhimu kuwajali wagonjwa wenye magonjwa sugu kama saratani, kiharusi, figo na Ukimwi ambayo huambatana na gharama kubwa za matibabu hasa kipindi cha corona kwa kuwa watu wanaoumwa magonjwa hayo wanakuwa kwenye hatari.

Aliiomba serikali kuhakikisha inatoa vibali vya dawa ya 'Morphine' kwenye hospitali mbalimbali kwa kuwa dawa hiyo ni muhimu katika kupunguza maumivu hasa kwa wagonjwa wa saratani.

"Dawa ya Morphine inatolewa katika vituo 65 kati ya 7,000 vilivyopo nchini vya serikali na binafsi, hii dawa ni muhimu kuna watu hawapati usingizi wanajisikia maumivu makubwa wakipata dawa hii inawasaidia kwa kiwango kikubwa," alisema.

Aliongeza: "Wahudumu wa tiba hii hawa vifaa vya kujikinga (PPE) kipindi hiki cha Covid-19, wamekuwa wakishindwa kwenda kutoa huduma kwa wagonjwa wetu, pia kuna changamoto kwenye kuthibitisha hivi vifaa vinavyotengenezwa nchini, jambo ambalo linakwamisha jitihada za baadhi ya hospitali zilizoamua kutengeneza PPE kwa ajili ya wagonjwa wake."

Alimpongeza Rais Magufuli kwa kuwatoa hofu Watanzania katika janga la corona, jambo ambalo limesaidia kwa kiwango kikubwa kisaikolojia wananchi.

## Wamachinga 200 watengewa eneo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wadogo zaidi ya 200, waliokuwa wakifanya biashara holela kwa kuzagaa katika maeneo yasiyo rasmi ya stendi na pembezoni mwa soko la Sabasaba jijini Dodoma, wametengewa eneo watakalo litumia kufanya shughuli zao.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, alipokuwa akitoa elimu juu ya madhara ya kufanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi ambako kunahatarisha afya zao na biashara yao.

Yuna aliwataka wafanyabiashara hao kuheshimu maelekezo ya jiji ambayo yanayowaonya kutofanya biashara bila kufuata utaratibu uliowekwa na mamlaka husika.

Alisema kitendo wanacho fanya cha kupanga bidhaa katika maeneo ambayo hayako rasmi wanaweza kupata hasara hivyo wanatakiwa kuheshimu na kuondoka mara moja na kuhamia eneo walilotengewa.

"Inasikitisha kuona soko na stendi iliyopo ndani ya Sabasaba halina mpangilio wa uwekaji wa biashara, na hata kwa upande wa magari kutokana na kila mmoja kukaa bila mpangilio, huku wengine wakijianzishia masoko pembezoni mwa soko na wengine wakiziba njia za waenda kwa miguu na vyombo vya moto," alisema na kuongeza:

"Kamwe sitokuwa tayari kuona uzembe huu ukiachwa, hivyo lazima mwondoke na mlio wengi mna meza zenu humu ndani ya soko."

Mmoja wa wafanyabiashara anayefanya shughuli zake kwenye stendi ya daladala ya Sabasaba alisema kuwa wanalazimika kuvamia maeneo hayo yasiyo rafiki kwa biashara kwa ajili ya kuwafuata wateja.

Naye Katibu wa soko hilo, Abuu Omary, alisema mfumo wa masoko ni biashara kuwekwa kwenye mpangilio kwa mujibu wa maelekezo na siyo kwa kuvamia kama ilivyo kwa wafanyabiashara wa eneo hili ambalo wapo kwenye hatari na hairuhusiwi.

Alisema kutokana na zoezi ambalo limefanyika la kuwatengea eneo mbadala ni imani yake sasa uvamizi wa masoko ya pembezoni utakwisha na hata wanaopanga maeneo ya stendi pia wataondoka ili kupisha magari ambayo yalikuwa yakikanyaga bidhaa kwa ajili ya msongamano wa watu.



Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Msalato, Neema Maro (kulia), akipokea msaada wa vifaa vya shule zikiwamo kalamu, rula, vifutio na vichongeo kutoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Wilaya ya Dodoma Mjini, Winifrida Kaliyo (kushoto), kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha sita wa shule hiyo, juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kalemani aipa EWURA siku saba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Merdad Kalemani, ametoa siku saba kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (EWURA) kufanya msako kwa wafanyabiashara wakubwa wa mafuta wanaoficha bidhaa hiyo ili kuuza kwa bei ya juu baadaye.

Aidha, Kalemani imeiagizi EWURA kuwachukulia hatua kali za kisheria ikiwamo kupigwa faini ya Sh. milioni 100 au kuwafutia leseni wote watakaobainika.

Waziri huyo aliipa EWURA siku saba kufanya msako kwa wafanyabiashara hao, ambao wanaficha mafuta hayo kwa lengo la kuuza baadaye mafuta hayo yatakapoadimika.

"Nawaagiza EWURA kufanya masako kwa wafanyabiashara wanaoficha mafuta kwa lengo la kuuza baadaye. Soko la mafuta litakapopanda, na yeyote atakayekamatwa achukuliwe hatua kali," alisema waziri huyo.

Dk. Kalemani alisema hivi sasa katika soko la dunia bei ya mafuta imeshuka, hivyo wafanyabiashara hao wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei elekezi ya serikali.

Aidha, alisema wafanyabiashara wadogo wameanza kuhaha kusaka mafuta baada ya wafanyabiashara wakubwa kuficha mafuta hayo ili baadaye bei itakapopanda wauze kwa bei ya juu.

Waziri huyo alisema wakibainika wafanyabiashara wakubwa wanaofanya michezo hiyo watachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo faini ya Sh. milioni 100, au kufutiwa leseni ya biashara hiyo.

"Natoa onyo kwa yeyote atakayekamatwa kwa tuhuma za kuficha mafuta atachukuliwa hatua za kisheria, ikiwamo kutoa faini ya Sh. milioni 100 au kufutiwa leseni ya biashara hiyo," alisema Dk. Kalemani.

Hata hivyo, Dk. Kalemani aliwaondoa hofu Watanzania kuwa serikali imehifadhi mafuta ya kutosha hata baada ya miezi mitatu, hivyo hakuna haja ya kuficha mafuta.

"Niwaondoe wasiwasi Watanzania serikali ina mafuta ya ziada lita milioni 386.9 ambazo zinaweza kutosheleza hata baada ya miezi mitatu mbele, hivyo hakuna haja ya watu kuficha mafuta," alisema Dk. Kalemani.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara wa mafuta kutumia bandari zote tatu Dar es Salaam, Tanga na Mtwara kufuata mafuta, ili kuepuka msongamano wa magari wanapoenda kuchukua mafuta.

Katika hatua nyingine, waziri katika kuimarisha hali ya mafuta vijijini, EWURA inatarajia kuanza kufungua vituo vidogo vya mafuta vijijini ili kuondoa adha ya upatikanaji.

"Tunalenga kupeleka mpango huo katika vijiji ambavyo havifikiki kwa urahisi kutokana na miundombinu ya barabara kuwa mibovu, hii ni kutaka kuwasaidia wale wanaonunua mafuta katika vidumu vya maji,"

# Wafanyakazi waidai kampuni ujenzi jengo la abiria mil. 47/-

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAFANYAKAZI 17 wa Kampuni ya DB Shapriya yenye makao yake jijini Dar es Salaam iliyokuwa imepewa kandarasi ya ujenzi wa jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa mkoani Mbeya (SIA), wameiomba serikali kuingilia kati ili walipwe mishahara yao zaidi ya miezi 10 ambayo kampuni hiyo haikuwalipa kabla haijavunja mkataba wake na serikali.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana, walisema kuwa wanaidai kampuni hiyo kiasi cha shilingi milioni 47.6 ambazo ni malimbikizo ya mishahara yao ya miezi 10.

Mmoja wa wafanyakazi hao, Barberina Mtaba, alisema baada ya kampuni hiyo kuvunja mkataba wake na serikali imewatelekeza bila kuwalipa na hawaoni dalili yoyote ya wao kupata stahiki zao.

"Nilifanya kazi kwenye mazingira magumu kutokana na ujauzito, viongozi wa kampuni ya DB Shapriya walinitaka niendelee kuchapa kazi bila kuchukua tahadhari yoyote juu ya hali yangu licha ya kazi ngumu, hali iliyosababisha nipoteza maisha ya watoto wangu mapacha nilipokuwa najifungua," alisema Mbata.

Aliongeza kuwa tangu Juni 30, mwaka 2018, waliambiwa na viongozi wa kampuni hiyo vibarua wote kuacha kazi hadi sasa hawafahamu nini hatima ya kupewa malipo yao.

Diamond Mwaijande alisema kutokana na hali hiyo walilazimika kufika ofisi ya Meneja ya Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) Mkoa wa Mbeya, pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, lakini hadi sasa hawajasaidiwa.

Kaimu Meneja wa Tanroads, Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Divael Njoro, alikiri kupokea malalamiko ya wafanyakazi hao na kuyafikisha ngazi za juu na kwamba wanaendelea kufuatilia ili watumishi hao waweze kulipwa.



Meneja wa Taasisi ya Tulia Trust, Jacqueline Boaz (kulia), akiwakabidhi msaada wa sare za kazi kwa ajili ya madereva wa bodaboda wa Kata ya Mwansekwa, zilizotolewa na taasisi hiyo, jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA.**

# TRA yatembelea walipakodi kuwapa elimu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imeanza kutembelea wafanyabiashara kuwapatia elimu ya mlipakodi pamoja na umuhimu wake katika kukuza uchumi wa nchi pamoja na maendeleo ya mtu mmoja mmoja.

Kaimu Meneja wa Elimu kwa Mlipakodi wa mamlaka hiyo, Steven Kauzeni, alisema jana kuwa tayari mamlaka hiyo imeanza ziara ya kutombelea wilaya zote za Mkoa wa Mbeya kwa lengo ya kuwafikia wafanyabiashara mlango kwa mlango kuwapa elimu ya masuala ya kodi.

Alisema katika maeneo wanayoyatembelea watahakikisha wanatoa nafasi kwa wafanyabiashara kuzungumzia vikwazo vinavyowakabili katika suala la kulipa kodi na wao wanavitolea ufafanuzi vikwazo hivyo.

Kauzeni alisema wakati wa kuelekea kumaliza mwaka wa serikali ambao ni Juni 30, wanatamani kila mfanyabiashara awe tayari amekwishakulipa kodi yake ili kuepukana na foleni katika kipindi hiki cha janga la ugonjwa wa corona.

"Tulianza kampeni ya mlango kwa mlango Dar es Salaam kwa kuwatembelea wafanyabiashara na sasa tuko hapa jijini Mbeya eneo la Mji wa Mbalizi tuwazungukia wafanyabiashara wetu kuwahamasisha waendelee kulipa kodi kwa wakati ili hizo kodi ziendelee kuboresha huduma za kijamii ikiwamo ujenzi wa barabara, hospitali na shule," alisema Kauzeni.

Aliwahamasisha wafanyabiashara kuendelea kujenga uhusiano mzuri na maofisa wa TRA, ili kupata ushauri wa kitaalamu katika ulipaji wa kodi na mafanikio kibiashara.

Mmoja wa wakazi wa Mji wa Mbalizi ambao waliotembelewa na maofisa wa mamlaka hiyo, Ambakisye Kibona, alisema ni uamuzi wa busara umefanywa kuwatembelea mlango kwa mlango wafanyabiashara kwa madai kuwa itasaidia wajione ni sehemu mamlaka na wanathaminiwa.

Aliongeza kuwa kitendo hicho kitawasiadia kupata maarifa zaidi juu ya namna ya kulipa kodi, lakini kuhoji mahali ambapo hawapaelewi.

Elia Nyika, alisema kitendo cha maofisa hao kuwatembelea kimesababisha waongeze ari ya kulipa kodi kwa wakati kwani ametambua umuhimu wa kulipa ili kuleta maendeleo kwenye jamii inayomzunguka.

# Machinga walalamika Jiji kutelekeza mnada

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAMACHINGA katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya wameulalamikia uongozi wa Jiji kwa madai ya kutelekeza mnada wa kila Jumamosi, ambao ujenzi wake uligharimu zaidi ya Sh. milioni 150.

Eneo hilo la mnada kwa sasa limegeuka kuwa maficho ya vibaka na wezi.

Mnada huo uliopo katika eneo la uwanja wa ndege wa zamani ulijengwa mahususi kwa ajili ya wamachinga na wajasiriamali wadogo, huku wakiahidiwa kuboreshwa kwa miundombinu ikiwamo ujenzi wa stendi mpya ya mabasi yaendayo mikoani.

Wakizungumza na Nipashe, machinga hao walisema mnada huo umegeuka kuwa mazalia ya wadudu hatari wakiwamo nyoka baada ya wajasiriamali kusita kufanya biashara zao katika eneo hilo.

Mmoja wa machinga hao, Silia Kabale, alisema ujenzi wa mnada huo ni agizo la Rais John Magufuli alilolitoa mwaka 2019 alipokuwa kwenye ziara mkoani Mbeya ambapo katika Uwanja wa Ruanda Nzovwe aliagiza eneo la Uwanja wa Ndege wa zamani utumike kwa ajili ya shughuli za kibiashara.

Kabale alisema baada ya agizo hilo, viongozi mbalimbali wakiwamo wa Mkoa na Jiji walilitembelea na kutoa maagizo mbalimbali juu ya kuboresha eneo hilo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vizimba.

"Kwa sasa eneo hili hakuna machinga yeyote anayefanyia kazi hapa, kwa sababu miundombinu yake haielewi hali iliyosababisha nyasi kuota ndani ya vibanda bila kufanyiwa usafi na giza linapoingia eneo hili hugeuka kuwa maficho ya wezi na wahalifu na sio wamachinga wala wajasiriamali wanaoonekana hapa kufanya biashara," alisema Kabale.

Akizungumzia hali hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Saad Mtambule, alisema wamachinga wabishi kuhamishia shughuli zao kwenye eneo hilo licha ya miundombinu kuwa rafiki kwao.

Alisema uongozi wa halmashauri kila mara umekuwa ukiwahamasisha kuhamia hapo, lakini baadhi yao wanakaidi na kuendelea kufanya biashara za kuhamahama.

Hata hivyo, aliahidi kuwa wataendelea kuboresha miundombinu ili wajasiriamali na machinga wote wahamie kwenye eneo hilo, ambalo Rais Magufuli aliamuru liwe kwa ajili yao.





# Wafurahia kufutwa tozo 20 kwa 'Wamachinga'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUFUATIA kufutwa kwa tozo na ada 20 zilizokuwa zikitozwa kwa wafanyabiashara wadogo (mamalishe) pamoja na wawekezaji wa sekta ya utalii na uwekezaji, wadau mbalimbali wameipongeza Serikali ya Zanzibar kwa uamuzi huo.

Miongoni mwa tozo zilizofutwa ambazo zimewalenga watu wa kipato cha chini ni wafanyabiashara mamalishe ambao walikuwa wakipata usumbufu wa kulipa kwa siku Sh. 1,000 hadi 2,000 kutoka kwa viongozi wa serikali za mitaa.

Katika bajeti iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa kwa mwaka wa fedha 2020-2021, kundi la wafanyabiashara, mamalishe na wafanyabiashara wa juakali maarufu 'Wamachinga' sasa watatozwa Sh. 30,000 kwa mwaka pamoja na kupewa vitambulisho rasmi vinavyowatambulisha kuwa ni walipa kodi.

"Nimeisikia bajeti ya serikali ambayo imetutaja moja kwa moja sisi wafanyabiashara wadogo kupunguziwa tozo na sasa kupewa vibali ambavyo vitatuwezesha kufanya biashara zetu kwa ufanisi wa hali ya juu," alisema Husna Bakari, mamalishe.

Alisema moja ya kero kubwa iliyokuwa kikwazo katika kutekeleza majukumu ya biashara ni usumbufu waliokuwa wakiupata kutoka kwa wafanyakazi wa Manispaa ya Mji wa Zanzibar na kuwalazimu kukimbia kila siku na kutoa rushwa.

Khamis Juma, mfanyabiashara anayejishughulisha na kuuza mahindi ya kuchoma katika eneo la Darajani, Unguja, alisema wamefurahishwa na uamuzi wa kuwapatia vitambulisho rasmi ambavyo vitawaondolea usumbufu wa kufukuzana na wafanyakazi wa Manispaa.

"Tumefurahishwa na uamuzi huo ambao sasa utatuwezesha sisi wanawake kufanya shughuli zetu za kujipatia riziki bila ya matatizo wala usumbufu kutoka kwa wafanyakazi wa Manispaa baada ya kupewa vibali," alisema.

Kwa upande wa wakulima wa kilimo cha mwani katika kijiji cha Jambiani kati ya Unguja wamefurahishwa na bajeti hiyo ambayo sasa imewapunguzia mzigo wa kukatwa ada ya Sh.1,000 kutokana na kiwango wanaouza kwa uongozi wa serikali za mitaa.

"Ipo tozo ya Sh. 1,000 wakati mwingine tunakatwa na kwenda kwa serikali za mitaa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambayo hulingana na kiwango cha mwani tunachouza kwa matajiri," alisema.

Mfanyabiashara anayesafirisha mwani kwenda nchi za Ulaya hadi Marekani, Abdalla Batashi, kutoka kampuni ya Sea Weed, alisema zimekuwapo tozo na kodi mbalimbali alizokuwa akitozwa kuanzia katika serikali za mitaa hadi usafirishaji wa zao hilo ambazo baadhi yake zimekuwa sawa na usumbufu kwa sababu hazifahamiki na hazipo kisheria.

"Nimefurahishwa na uamuzi wa kufuta kodi zilizokuwa nikitozwa katika hatua ya awali ya kuanzia ununuzi hadi usafirishaji ambazo baadhi yake hazipo kisheria," alisema.

Kwa upande wao, wasomi na wachumi wa Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) na taasisi za fedha wameipongeza bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufuta zaidi ya tozo na ada 20 zilizokuwa zikitozwa kwa wafanyabiashara wadogo, mamalishe, juakali pamoja na wawekezaji wa sekta ya utalii.

Mhadhiri wa SUZA, Dk. Sikujuwa Omar, alisema bajeti hiyo imelenga kuwakomboa wafanyabiashara wa chini ili wapige hatua kubwa ya maendeleo.

Alisema zilikuwapo kodi na tozo nyingi zilizokuwa zikiwakabili wafanyabiashara hao kiasi ya kuyumba katika utendaji wa biashara zao na kurudi nyuma.

"Nimefurahishwa na bajeti ya serikali iliyowasilishwa na Balozi Mohamed Ramia ambayo imelenga kuwakomboa wafanyabiashara wadogo kufanya kazi zao kwa ufanisi na kuondokana na usumbufu uliokuwa ukiwapata awali," alisema.

Ofisa Mwandamizi wa Idara ya Uchumi kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar (BPZ), Saleh Hijja, aliipongeza bajeti hiyo licha ya kuyumba kwa uchumi kutokana na ugonjwa wa Covid-19, serikali ipo imara kiuchumi na kulipa mishahara kwa wakati pamoja na pensheni kwa wastaafu.

Aliipongeza bajeti hiyo kwa kuwapunguzia kodi na tozo wafanyabiashara wadogo na wajasiriamali ili waweze kupiga hatua kubwa ya maendeleo na uzalishaji mali.

"Hii ni bajeti iliyojikita kuwakomboa wanyonge na wajasiriamali na kuona wanaendelea na juhudi zao za uzalishaji mali na kupambana na umaskini," alisema.




Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Balozi Muhamed Ramia, akionyesha mkoba wakati akiingia katika ukumbi wa Baraza la Wawakikishi, Chukwani juzi, kwa ajili ya kuwasilisha bajeti ya serikali kwa mwaka 2020/2021. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Jamii yatakiwa kuweka mazingira rafiki kwa watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Maudline Cyrus Castico, amesema jamii inapaswa kuweka mazingira rafiki ya upatikanaji wa haki za watoto bila kuathiri ustawi wao wa maisha ya kila siku.

Castico aliyaeleza hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu na maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, ofisini kwake Mwanakwerekwe Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema utekelezaji wa haki za watoto ni msingi imara unaohitaji kutengenezewa mazingira ili ziweze kupatikana kama zinavyotakiwa.

"Kwa kutekeleza hayo tutakuwa tumeisaidia serikali, jamii, familia na vizazi vyetu kujenga mifumo endelevu ya upatikanaji wa haki hasa ukijumuishwa na malezi bora ya familia," alisema.

Hata hivyo, alisema maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yamewafikia wakiwa wapo kwenye kipindi kigumu cha maradhi ya corona na kuwanyima fursa ya kuwa pamoja ya kuitafakari, kujitathmini utekelezaji wa mikakati ya kuimarisha ustawi wa mtoto.

Alisema pamoja na kujitokeza hali hiyo, aliitaka jamii kuimarisha familia kwa kuwadhibiti watoto wao ili kuwaepusha na maradhi hayo na vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhidi yao.

Alizitaka taasisi na jamii kuwa karibu na watoto wao ili kuwalinda na watu wenye nia ovu ndani ya jamii yao na kuwa hilo litasaidia kutambua viashiria vyote vya ukatili na udhalilishaji wa aina zote na kujenga jamii bora.

Pia, alisema kuwa watoto wanahitaji mapenzi, ukaribu na kujengewa uthubutu wa kuzungumza na wazazi na watu wengine ndani ya familia ili kuwaepusha na matendo yote yanayoweza kusababisha au kuchochea kuharibu upatikanaji wa haki zao za msingi.

"Napenda kusisitiza kuwa suala la malezi bora ni msingi bora wa mwanzo ambao unawajenga watoto, mfano haki ya kulindwa, kuishi na ushiriki na ushirikishwaji wa watoto kwa masuala yanayowahusu ili kufikia ndoto za maisha yao," alisema.

Alisema kuwa ni jukumu la wote kuhakikisha watoto wao wanalindwa, wanatunzwa na kuendelezwa ili kuwa na taifa bora.

Alisema kuwa bila ya kuwekeza nguvu kazi ya kutosha katika hilo watakosa fursa ya kuendelea kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa kukosa watu wenye utashi na utetezi wa taifa lao na pia watajenga taifa la watu wasiojitambuwa jambo ambalo ni baya.

## Balozi apokea vifaa ujenzi vya mil. 10/- kutoka NMB

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amepokea vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 10 kutoka Benki ya NMB kwa lengo la kuendeleza shule katika Jimbo la Kikwajuni.

Katika msaada huo kuna mabati 215 pamoja na mbao 333 za kujengea kwa ajili ya shule za Kidutani, Jang'ombe na Miembeni kwenye jimbo hilo la Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni.

Balozi Iddi alisema, anaishukuru benki hiyo kwa kurudisha kiasi cha faida kwa jamii na kuisaidia serikali kutimiza majukumu yake katika sekta mbalimbali nchini.

"Tunashukuru msaada huu umekuja wakati muafaka, pia nawapongeza wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa kazi kubwa mliyoifanya. Wakati huu ambapo tunajiandaa na uchaguzi mkuu nawaomba msijiingize kwenye masuala ya rushwa, fanyeni kazi zenu kwa weledi na kampeni ziwe za kistaarabu," alisema Balozi Iddi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wateja Wadogo Benki ya NMB, Filbert Mponzi, alisema misaada hiyo ni sehemu ya shughuli zao za kijamii na daima wanatoa asilimia moja ya faida wanayopata kwa kusaidia masuala mbalimbali ya kijamii.

"Huu ni wajibu wetu, tunaangalia namna nzuri ya kuinufaisha jamii tunayofanya nayo kazi, tunasaidia masuala ya afya, elimu na wakati wa majanga ya asili," alisema Mponzi wakati wa kukabidhi vifaa hivyo.

Naye Naibu Waziri Masauni kwa niaba ya wananchi wa jimbo lake, aliishukuru NMB kwa msaada walioutoa na ambapo alibainisha kuwa watautendea haki ili kuondoa changamoto wanazokumbana nazo kwenye jimbo hilo kwa kushirikiana na mwakilishi Nassor Salim Ali, ikiwamo changamoto za majisafi na salama, barabara na kuhakikisha watu wenye umri mkubwa wanaishi kwa furaha na amani.

Katika hatua nyingine Benki ya NMB imetoa msaada wa vifaa mbalimbali kwa ajili ya tiba vyenye thamani ya jumla ya Sh. milioni 3.4 kwenye maeneo mbalimbali ya kisiwa hicho. Wafanyakazi wa benki hiyo katika matawi ya Malindi na Mwanakwerekwe, walitoa msaada wa vifaa mbalimbali kituo cha afya Tunguu vyenye thamani ya Sh. milioni 2.7 ni vifaa vya majisafi na salama, tiba na vitenganishi.

Katika hatua nyingine wafanyakazi wa Tawi la Chakechake, Pemba, wametoa vitu mbalimbali vyenye thamani ya Sh. 700,000 kwa uongozi wa Wizara ya Afya Pemba, kwa ajili ya kuadhimisha Siku ya Uchangiaji Damu Duniani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NAFASI ZA KAZI**

**NAFASI ZA KAZI YA DEREVA NA MAUZO** Mwenye uzoefu wa kuuza Maji. PIga simu namba : **0767 269677 saa za kazi**

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.30 OF 2020**

**In the matter of the Estate of the late FELIX ZACHARIA KANWA of Line Police within Dodoma City**

**AND**

**In the matter of application for letters of Administration by ADELINA GASPAR MKULASI**

**GENERAL CITATION**

***(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)***

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 07th Day of July 2020.

Dated at Dodoma this 15th Day of JUNE 2020.

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU DODOMA**

**SHAURI LA JINAI MAOMBI NA.74/2019**

**MKURUGENZI WA MASHTAKA(DPP)...............................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**KASHINDE ALEX LUSANA...................................MJIBU MAOMBI**

**KWA: KASHINDE ALEX LUSANA**
**POPOTE PALE ULIPO**

**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA JINAI MAOMBI NA 74/2019**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA:** shauri tajwa hapo juu litatajwa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma mbele ya **MHE. JAJI GEORGE M. MASAJU,** wa Mahakama kuuya Tanzania Dodoma, saa tatu (3.00)Kamili asubuhi siku ya alhamisi tarehe 9/7/2020.
HIVYO: Unatakiwa ufike wewe Mwenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

**NA ENDEPO:** hutafika wewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itavyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.

**IMETOLEWA:** Kwa mkono wangu na mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 8/6/2020.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOMA

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA CHATO**

**MAHALI LILIPO CHATO**

**MAOMBI/RUFAA NA. 19 MWAKA 2020**

1. **SAMWELI JACOB**
2. **JOSEPH MANAMBA.................................MWOMBAJI/MRUFANI**
3. **CHARLES NGEZE**

**DHIDI YA**

1. **PANGEA MINERALS TRAWAKA LTD**
2. **B'MULO DISTRICT COUNCIL & OTHER**

## WITO/KUITWA SHAURINI

**KWA:**
1. **PANGEA MINERALS TRAWAKA LTD**
2. **B'MULO DISTRICT COUNCIL**
3. **MAVOTA VILLAGE COUNCIL**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutaja/kusikilizwa tarehe 23rd Mwezi June, mwaka 2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya **MH. BAHATI COLEX NDAMBO** Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa pamoja na utetezi/majibu yako ndani ya siku 21.
**AMRI** hii imetolewa leo kwa mkono wangu na Lakiri/Mhuri wa Baraza hii leo tarehe 16th Mwezi June, Mwaka 2020.

MWENYEKITI

115777102

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NANYUMBA YA WILAYA MBEYA**

**SHAURI NO. 11/2020**

**DEBORA RAMADHANI NYAMIZI.......................MADAI**

**DHIDI YA**

1. **EMANUEL JORAM KASEKWA...........................MDAIWA**
2. **FINCA MICROFINANCE LTD...........................MDAIWA**
3. **PETER MUHEZYA MBOYA ...............................MDAIWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA: EMANUEL JORAM KASEKWA**

Fahamu kwamba mdai amefungua madai dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kwa ajili ya kutajwa tarehe 9/07/2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh. T Munzerere Mwenyekiti wa Baraza. Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenywe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria. Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya Mjini.
Kumbuka: usipoudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 15/06/2020

T.Munzerere
Mwenyekiti
15/06/2020

115777402

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**

**SHAURI LA MADAI NAMBA 12 LA MWAKA 2020**

**AMANA BANK LTD................................ MDAI**

**DHIDI YA**

**BARIKI ELIAS MUSHI...............................MDAIWA**

**KWA: BARIKI ELIAS MUSHI**

**POPOTE ULIPO**

Mahakama hii inakufahamisha kwamba MDAI amefungua shauri la MADAI dhidi yako nakala yake inapatikana Mahakama hii.
Shauri limepangwa kusikilizwa Mmamo tarehe 17/06/2020 Saa 2:00 asubuhi na unatakiwa kuwepo, au kuwakilishwa kisheria pamoja na kuleta utetezi wako dhidi ya maombi haya.
Zingatia kwamba kutokufika kwako tarehe hiyo, shauri litaanza kusikilizwa bila ya wewe kutaarifiwa tena, na maamuzi kutolewa.
Imetolewa kwa mkono wang una mhuri wa mahakama hii leo tarehe 11/06/2020

..........................................
**HAKIMU MKAZI**
**MWANZA**

115777302

---

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
16/06/2020

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATANO tarehe17/06/2020** kampuni ya **SKOL BUILDING CONSTRACTORS LTD** itasafirisha Mzigo wake Excuvator. Kutoka **TABATA kuelekea SINZA** kupitia **LUGOBA/MAZIZI,** Gari hilo yana namba za usajili: **HORSE NO-T167 CMY/TRELA NO. T592 CLG**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **20** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.0** |
| **Kimo** | - | **mita** | **50** |

3. Njia itakayotumika: **ISHEKILANGO RD hadi BAGAMOYO MSATA** . Gari litasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115776802

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

*Kwa Habari Motomoto usikose*

*Gazeti lako la Nipashe*

*kila siku Tupigie 0782253676*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Ufaransa yatangaza kufungua shule, vyuo vikuu Juni 22

**PARLIS, Ufaransa**

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron ametangaza kuondoa vizuizi vya kiuchumi vilivyowekwa ikiwamo kufunguliwa kwa migahawa, shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu.

Katika hotuba yake ya nne kwa njia ya televisheni, Rais Macron alitangaza kuondoa vizuizi hivyo tangu kulipozuka ugonjwa wa corona.

Kwenye hotuba yake hiyo usiku wa kuamkia jana, Rais Macron alisema nchi yake imepata ushindi wa kwanza dhidi ya ugonjwa wa corona na kwamba migahawa katika mji wa Paris na viunga vyake itafunguliwa ili watu wale wakiwa ndani kuanzia jana, tofauti na hapo awali ambapo wateja waliruhusiwa kuketi nje ya migahawa.

"Kufikia sasa ninatangaza kwamba migahawa na maduka itafunguliwa tena nchini kote isipokuwa Guyana na Mayotte, ambapo virusi bado vinaendelea kushika kasi. Na kuanzia Juni 22 wanafunzi wote wanatakiwa kurejea tena shuleni," alisema Rais Macron.

Kulingana na takwimu za hivi karibuni kutoka Wizara ya Elimu ya Ufaransa, wanafunzi milioni 1.8 kati ya milioni 6.7 - wamerejea shuleni.

Vilevile, kwenye vyuo vikuu, wanafunzi 600,000 wamerejea kati ya milioni 3.3.

***RFI***



vikosi vya kijeshi vya serikali ya kitaifa nchini Libya vikiwa katika moja ya doria. **PICHA: ALLIANCE**

# Afrika yataka uchunguzi ukatili wa polisi Marekani

**GENEVA, Uswisi**

BARAZA la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa leo linatarajiwa kujadili suala la ukatili wa Jeshi la Polisi wa Marekani dhidi ya watu weusi.

Nchi za Afrika zinapigia debe kuanzishwa uchunguzi kuhusu ubaguzi wa kimfumo na ukatili wa polisi nchini Marekani na kwingineko, zikilenga kutetea haki za watu wenye asili ya Afrika.

Waraka uliozungushwa miongoni mwa wanadiplomasia mjini Geneva unaelezea kushtushwa kwa nchi za Kiafrika, na visa vya ukatili vinavyofanywa na polisi dhidi ya watu waliokuwa wakiandamana kwa amani.

Pia unapinga kifo cha Mmarekani mweusi, George Floyd aliyekufa akiwa mikononi mwa Polisi mjini Minneapolis.

Kifo chake kilifuatiwa na maandamano makubwa katika sehemu nyingi za dunia, kupinga ukatili huo.

Mwakilishi wa Burkina Faso katika Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa mjini Geneva, Desire Sougouri, alisema tatizo hili la ubaguzi dhidi ya watu wenye asili ya Afrika limo katika majukumu ya baraza hilo, na linapaswa kuchunguzwa.

''Kwa bahati mbaya, kifo cha George Floyd siyo tukio pekee, kwa sababu watu wengi weusi wanakutwa na madhila yale yale kila siku katika sehemu nyingi za dunia. Wanakumbwa na ukatili wa polisi kwa sababu tu ya asili yao. Itakuwa haieleweki ikiwa baraza hili halitalishughulikia tatizo hilo,'' alisema Sougouri.

Alisema hiyo ndiyo sababu mataifa ya Afrika yanalitaka baraza hilo kuanzisha haraka mjadala kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu kwa misingi ya rangi ya ngozi, ubaguzi wa rangi wa kimfumo, na ukandamizaji wa polisi dhidi ya watu wenye asili ya Afrika wanaoandamana kupinga unyanyasaji dhidi yao.

Marekani inayolengwa katika waraka huo sio mwanachama tena wa Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa. Ilijiondoa miaka miwili iliyopita, ikidai baraza hilo lina uhasama dhidi ya Israel ambaye ni mwandani wa Marekani.

Bado Washington hawajatoa tamko lolote kuhusu hatua hiyo ya kuwekwa kizimbani.

Maudhui ya waraka wa nchi za kiafrika, ambayo yanaweza kurekebishwa baada ya mazungumzo ndani ya baraza, yanataka iundwe tume huru ya kimataifa itakayofanya uchunguzi wa masuala yanayohusu mifumo ya ubaguzi, uvunjaji haramu wa haki za msingi za binadamu, unyanyasaji dhidi ya watu weusi nchini Marekani na maeneo mengineyo duniani.

Tume hiyo itachunguza pia namna serikali na tawala za kimajimbo zinavyoshughulikia maandamano ya amani, pia tuhuma za kutumia nguvu za ziada dhidi ya waandamanaji, waandishi wa habari.

Marekani na nchi nyingine zimetakiwa kutoa ushirikiano kamili na tume hiyo, inayopaswa kuchapisha ripoti yake baada ya mwaka mmoja.

***DW***

# Marekani yalaumiwa kwa mauaji ya raia Somalia

**MOGADISHU, Somalia**

RIPOTI mpya ya Shirika la Utetezi wa Haki za Binadamu la Human Rights Watch limesema, mashambulizi mawili ya anga yaliyofanywa na Marekani mapema mwaka huu yamewaua raia saba nchini Somalia.

Shirika hilo la Human Rights Watch limesema Jeshi la Marekani halikufanya uchunguzi wa kina kwa shambulizi lake la Februari 2, ambalo limemuua mwanamke mmoja akiwa nyumbani kwake. Na baadaye la Machi 10 ambalo limeangamizia maisha ya wanaume watano na mtoto mmoja.

Uchunguzi wa shirika hilo, haukubaini ushahidi wowote katika mashambulizi yote mawili, wa lengo la kijeshi katika kukabiliana na kundi la wenye itikadi kali za dini ya Kiislamu, lenye kujihami na silaha la Al-Shabab.

Hakuna kamandi ya kijeshi ya pamoja kati ya Marekani na Afrika (AFRICOM) wala serikali ya Somalia ambao wamewasiliana na familia kwa lengo kuthibitisha kitendo hicho cha mauaji ya raia au kutathmini madai hayo kwa lengo la kujirekebisha.

Kati ya Februari na Mei, Shirika la Human Rights Watch lilifanya mahojiano kwa njia ya simu na watu 14, wakiwamo ndugu na jamaa wa waliouawa katika kipindi cha Februari na Machi kwamba wanne miongoni mwao walifika katika eneo la tukio, muda mfupi baada ya maafa na kutoa taarifa za kina.

Katika ripoti kuhusu athari ya operesheni ya kivita nchini Somali kwa raia Aprili 27, mwaka huu, AFRICOM ilisema ilichunguza matukio 20 ya anga ambayo yalidaiwa kusababisha maafa kwa wananchi kati ya Februari na Machi na kwamba katika kipindi hiki bado wanachunguza mengine saba.

Miongoni mwa matukio hayo ni pamoja na ambayo shirika hilo la haki za binadamu linasema limeyachunguza.

Katika hitimisho lake shirika hilo limetaka majeshi nchini Somalia kuacha mara moja kuwaua raia wasio na hatia. Na kuyahimiza kuwatambua kwa ukamilifu wale wanaoowalenga kabla ya kufanya mashambulizi.

**DW**

**Hakuna kamandi ya kijeshi ya pamoja kati ya Marekani na Afrika (AFRICOM) wala serikali ya Somalia ambao wamewasiliana na familia kwa lengo kuthibitisha kitendo hicho cha mauaji ya raia au kutathmini madai hayo kwa lengo la kujirekebisha.**

# LEVERKUSEN KUMBAKISHA HAVERTZ



**MUNICH, Ujerumani**

KAI Havertz anataka kuendelea mbele na kipaji chake sehemu nyingine "katika siku za hivi karibuni", lakini Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bayer Leverkusen, Fernando Carro, anataka kumuona kwenye viwanja vinavyofahamika.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, Havertz ameripotiwa kwamba anawaniwa na Real Madrid, Chelsea na Bayern Munich miongoni mwa nyingi, huku Leverkusen inamatumaini ya kumuuza kwa euro milioni 100.

Mkurugenzi wa Michezo, Rudi Voller alionyesha nia yake kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ambaye alisherehekea wiki iliyopita siku yake ya kuzaliwa, kubakia hapo kwenye dimba la BayArena kwa msimu mwingine.

Mkataba wa sasa wa Havertz unamalizika Juni 2022.

Carro anatambua kwamba Havertz anataka kuondoka haraka, lakini ana matumaini suluhisho litapatikana hivi karibuni.

"Klabu nyingi zinamwania Kai Havertz," Carro amesema alikiambia gazeti la Kolner Stadt-Anzeiger.

"Kai amekuwa na sisi kwa miaka 10. Naona mchezaji anataka kwenda sehemu nyingine kwa ajili ya hatua nyingine kwa siku za usoni. Na unatakiwa kuheshimu matakwa yake, lakini kwa sasa ana mkataba na sisi hadi mwaka 2022."



## GERRARD ATAKA KLOPP AJENGEWE SANAMU

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL inatakiwa kufanyia kazi ujenzi wa sanamu ya Jurgen Klopp haraka iwekanavyo mara tu ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya England, amesema gwiji wa klabu hiyo, Steven Gerrard.

Mlipuko wa virusi vya corona ulilazimika kusimama kwa msimu wa ligi tangu Machi mwaka huu Liverpool ikiongoza kwa pointi 25 kileleni na ushindi wa mechi mbili tu utawafanya washinde taji la Ligi hiyo kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1990.

Msimu wa 2019-20 utaendelea kuanzia Jumatano huku mechi zikicheza bila mashabiki uwanjani, wakati wanaoshika nafasi ya pili Manchester City wakicheza dhidi ya Arsenal.

Kipigo kwa timu hiyo ambayo ni bingwa mtetezi inayonolewa na kocha, Pep Guardiola kutawapa nafasi Liverpool kutwaa ubingwa kama wakishinda dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja, Everton pale Goodison Park Jumapili.

Nahodha wa zamani wa Liverpool, Gerrard hana shaka kwamba heshima ya kujengewa sanamu inamsubiri Klopp, ambaye alishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na klabu bingwa ya Dunia mwaka jana.

"Kwa kumjua Jurgen, anastahili heshima hiyo. Najua kwamba ni mtu mwenye heshima na mnyenyekevu na heshima," amesema Gerrard akiliambia gazeti la The Athletic.

"Ukiangalia kwenye mizani kwa kazi aliyoifanya, kwa uhakika kabisa anastahili kuwa mmoja wa makocha wenye sanamu.

"Kitu cha kukielewa ni kwamba wakati Jurgen akichukua Liverpool hawakukaribia kuwa timu bora nchini, hawakuwa hata kwenye nne bora.

"Kwa kile alichokifanya kwa Liverpool anastahili heshima kubwa zaidi, kwani hii ni mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 30 iliyopita."

Gerrard katika kipindi chake cha miaka 17 kucheza hapo alishinda mataji mawili ya FA, matatu ya EFL na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# Lewandowski: Sifikirii kuhusu Ballon d'Or

**MUNICH, Ujerumani**

ROBERT Lewandowski amesema haifikirii sana Ballon d'Or lakini "chochote kinawezekana" wakati linapokuja suala la kushinda tuzo hiyo.

Straika huyo wa Bayern Munich hajawahi kuwa kwenye tatu bora ya tuzo hizo kubwa zaidi binafsi kwa wachezaji, huku nafasi ya juu zaidi aliyowahi kuishika ni wakati alipomaliza kwenye nne bora mwaka 2015.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 anaonekana anaweza kuwa kwenye nafasi kubwa ya kuitwa tuzo hiyo mwaka huu 2020, akiwa amefunga mabao 45 kwenye mashindano yote msimu huu na kuiwezesha Bayern kushinda taji la Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, msimu huu.

Kama kikosi hicho cha kocha, Hansi Flick kitabeba taji la DFB-Pokal na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, Lewandowski anaweza kuwa na nafasi kubwa ya kushinda tuzo hiyo kwa mara ya kwanza dhidi ya Lionel Messi na Cristiano Ronaldo.

"Nilikuwa kwenye sherehe ya tuzo hizi Desemba mwaka jana," amesema Lewandowski akiliambia jarida la France Football.

"Tutaona. Ninachojaribu kufanya ni kuwa kwenye ubora wangu, kushinda mataji na kufunga mabao. Lakini kile ni kitu ambacho kinakuja kutokana na kubeba mataji mengi. Hicho ndio kitu muhimu zaidi.

"Sifikirii kuhusu Ballon d'Or, hata kama kwenye maisha naamini kila kitu kinawezekana."

## HABARI MICHEZO

# MODRIC:
## MBAPPE ONDOKA PSG UNG'ARE




**MADRID, Hispania**

KYLIAN Mbappe anatakiwa kuondoka Paris Saint-Germain ili kwenda kuonyesha kipaji chake kwenye ligi yenye ushindani mkubwa, kwa mujibu wa nyota wa Real Madrid, Luka Modric.

Akiwa bado ana umri wa miaka 21, Mbappe ameshinda mataji manne ya Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Coupe de France na Coupe de la Ligue, huku pia akibeba kombe la Dunia akiwa na Ufaransa miaka miwili iliyopita.

Madrid kwa muda mrefu imekuwa ikihusishwa na kuwania kumsajili Mbappe, ambapo atajikuta akifanya kazi chini ya gwiji wa Ufaransa na Los Blancos hao, Zinedine Zidane.

Mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Michezo wa PSG, Leonardo alisema haoni kama Mbappe au Neymar wataondoka klabuni hapo wakati wa dirisha la usajili linalokuja.

Lakini Modric anaamini Mbappe atahitaji kuondoka kama anataka kuwa mchezaji mkubwa duniani.

Akizungumza na gazeti la La Gazzetta dello Sport, Modric amesema: "Mbappe ana kila kitu kuweza kutawala soka la dunia hii, lakini nafikiri kwamba anatakiwa kwenda kwenye ligi ambayo timu yake haishindi kirahisi.

"Pia naona mambo mazuri kwa Vinicius Jr na nampenda (Kevin) De Bruyne na (Raheem) Sterling."

Mbappe bado ana nafasi ya kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, huku mashindano hayo yakitarajiwa kuendelea Agosti baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

## HAALAND KUTAFUTIWA PATINA DORTMUND

**DORTMUND, Ujerumani**

MTAZAMO wa Erling Haaland kwenye mechi na mazoezi unamfurahisha Lucien Favre tangu mshambuliaji huyo alipojiunga na Borussia Dortmund, lakini kocha huyo anataka yeye aelewe suala la kupumzika.

Haaland ameanza katika mechi tatu tu za Dortmund kwenye Bundesliga kati ya tano tangu msimu uliporudi tena mwezi uliopita, huku raia huyo wa Norway akiwa ameumia goti mwishoni mwa Mei.

Kiwango chake dhidi ya Schalke, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 hakikuwa kwenye ubora wake kama ilivyokuwa kabla ya mlipuko wa virusi vya corona, lakini bila ya uwepo wake Dortmund ilionekana kukosa kitu kwenye safu ya ushambuliaji.

Lakini Favre anafahamu kwamba pengo lake ni kubwa na Haaland ana mzigo mkubwa na hivyo anataka mshambuliaji mwingine asajiliwe msimu unaofuata ili kumwezesha nyota huyo wa zamani wa Salzburg kupata muda wa kupumzika.

"Nafikiri kila mtu anajua hilo," amesema Favre akiwaambia waandishi wa habari Jumatatu wakati alipoulizwa kuhusu usajili wa fowadi mwingine.

"Nafikiri hilo liko wazi, kwa sababu ndio kwanza ana umri wa miaka 19.

"Ni kawaida kwamba wakati mwingine anachoka, hivyo anahitaji muda wa kupumzika, na hilo ni lazima lifanyike."





## Mchango wa Messi Barca sio mabao tu - Setien

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Quique Setien, amesema Lionel Messi anatakiwa atambulike kwa mchango wake kwa timu ukiacha kufunga mabao, wakati akielekea kwenye kilele cha kipindi chake cha uchezaji.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina anahitaji mabao mawili tu kwa ujumla kufikisha 700 kabla ya mechi ya jana Jumanne, kwa klabu na nchi yake, baada ya kufunga moja wakati Barca ikiibuka na ushindi wa 4-0 dhidi ya Mallorca Jumamosi, mchezo wa kwanza tangu LaLiga kurudi tena baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Kocha Mkuu Setien anatambua mafanikio ya Messi - ambaye alicheza dhidi ya Mallorca licha ya kuonekana kuumia kwenye mazoezi na amesema nahodha huyo wa Barca anatakiwa kutambulika kwa mchango wake sio tu kwa mabao.

"Leo yupo poa. Hutakiwi kuzungumzia tu mabao yake anayofunga, lakini mchango wake kwa timu, kama kutoa pasi za mwisho. Hilo linatupa sisi pointi nyingi," amesema.

"Ni mchezaji wa kiwango chake kwa uhakika kabisa kufikisha mabao 700 sio jambo rahisi kwa mchezaji na ndio maana ni mchezaji bora duniani."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA: NAJIAMINI AUBAMEYANG ATABAKI ARSENAL MSIMU UJAO

●●● Asema ana uhakika na furaha kubakia klabuni hapo na...

**LONDON, England**

MIKEL Arteta anajiamini Arsenal inaweza kushawishi mshambuliaji Pierre-Emerick Aubameyang kuongeza muda wa kubakia na klabu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 mkataba wake wa sasa pale kwenye uwanja wa Emirates unamalizika Juni 2021 na ameiambia televisheni ya Telefoot kuwa uhamisho wake ujao "unaweza kuwa wa mwisho kwenye maisha yake ya soka".

Aubameyang pia alielezea kuhuzunishwa kwake kutokana na kushindwa kuendelea kwa mazungumzo ya kuongeza mkataba wake na Arsenal, ambako amefunga mabao 61 katika mechi 97 alizoichezea timu hiyo tangu alipojiunga nayo kutoka Borussia Dortmund Januari 2018.

"Tumekuwa na majadiliano mengi na Pierre, na familia yake na walaka wake. Nina uhakika kwamba tutapata njia sahihi ya makubaliano katika pande zote mbili," alisema Arteta kwenye mkutano wake na waandishi wa habari kuelekea mchezo wao dhidi ya Manchester City kesho Jumatano.

"Ni jukumu letu kumfanya ajisikie furaha ni njia sahihi kwa hatua yake inayofuata kwenye maisha yake ya soka.

"Kwa sisi kufanya hivyo, anahitaji kuhisi thamani yake. Nafikiri anahitaji kuhisi kwamba ni wa kwetu na tunamtaka, na kwa uhakika kabisa anahitaji kuamini tunaweza kuichukua klabu hii katika njia anayoitaka.

"Anakwenda kuwa mchezaji muhimu. Kwa wakati huu nina furaha kubwa namna gani kiwango chake kilivyo.

"Kwa uhakika nina uhusiano mzuri na yeye ambapo tunaweza kujadiliana mambo mengi uso kwa uso. Kwa kile ninachokijua hadi sasa, nafikiri ana furaha kuwa klabuni hapa."

Kuhusu hofu ya Aubameyang juu ya kuchelewa kwa majadiliano mapya, Arteta amebainisha kwamba hii inaweza kuwa rahisi na kutokana na mlipuko wa virusi vya corona kulifanya mambo mengi kutokwenda sawa.

"Kwa hali tofauti ni kwamba angependa kuona vitu vinafanyika kwa haraka," aliongeza.

"Kwa uhakika kabisa tulikuwa kwenye wakati muhimu wa mawasiliano. Lakini nina uhakika mkubwa kwamba anaweza kubakia na sisi na tunaweza kumshawishi."

## KWA UFUPI

**MAN YAMWANIA BAILEY**

MANCHESTER United inafikiria uhamisho wa pauni milioni 40 kwa winga wa Bayer Leverkusen na Jamaica, Leon Bailey mwenye umri wa miaka 22, kama usajili rahisi kuliko Waingereza wawili, Jadon Sancho wa Borussia Dortmund mwenye umri wa miaka 20, na kiungo wa Aston Vill, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 24. ***(Mail)***

**BAYERN NJIA NYEUPE KWA HAVERTZ**

BAYERN Munich ina nafasi nzuri ya kumsajili kiungo wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Kai Havertz mwenye umri wa miaka 21, mbele ya Manchester United na Chelsea, na pia wanamtaka winga wa Manchester City na Ujerumani, Leroy Sane mwenye umri wa miaka 24. ***(Telegraph)***

**TAKOWSKI AGOMBEWA LEICESTER, CRYSTAL**

LEICESTER City inapambana na Crystal Palace kuwania saini ya mlinzi wa kati wa Burnley na England, James Tarkowski mwenye umri wa miaka 27. ***(Mirror)***

**CHELSEA RASMI KWA TIMO WERNER**

UHAMISHO wa Timo Werner kutoka RB Leipzig kwenda Chelsea utakamilika rasmi wiki hii, wakati mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kipengele chake cha mkataba cha kununuliwa kwa pauni milioni 53 kumalizika jana Jumanne. ***(Evening Standard)***

**JUVE YAMTAKA JORGINHO**

KLABU ya Juventus inataka kumsajili kiungo wa Chelsea raia wa Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 28 na beki wa kushoto wa Hispania, Marcos Alonso mwenye umri wa miaka 29. ***(Express)***

**MAN CITY YAMWINDA HAKIMI**

MANCHESTER City inamfuatilia beki wa kulia wa Real Madrid na Morocco, Achraf Hakimi. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 kwa sasa anacheza kwa mkopo kule Borussia Dortmund. ***(AS)***

**SPURS YAMNYATIA MEUNIER**

KLABU ya Tottenham Hotspur ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili mlinzi wa Paris St-Germain na Ubelgiji, Thomas Meunier mwenye umri wa miaka 28, ambaye atakuwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu. ***(Express)***

**CHELSEA YAANZA MAZUNGUMZO NA BENRAHMA**

KLABU ya Chelsea imefungua mazungumzo ya kumsajili winga wa Brentford na timu ya taifa ya Algeria, Said Benrahma mwenye umri wa miaka 24. ***(RMC)***

**RONALDO AMPELEKA DE BEE MADRID**

KIUNGO wa zamani Uholanzi, Ronald de Boer amesema kiungo wa Ajax, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 23, itafaa kama akihamia Real Madrid kuliko Manchester United. ***(Marca)***

**MOURINHO KUMSAJILI THIAGO**

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho anataka kumsajili mlinzi wa Paris St-Germain na timu ya taifa ya Brazil, Thiago Silva mwenye umri wa miaka 35, akiwa mchezaji huru kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Sun)***

**ARSENAL YAJITUTUMUA KWA PARTEY**

KLABU ya Arsenal ipo tayari kumwongezea mshahara mara tatu kiungo wa Atletico Madrid na Ghana, Thomas Partey mwenye umri wa miaka 27, ili kumsajili. ***(Goal)***



## HABARI MICHEZO

# LIGI KUU ZANZIBAR KUREJEA JUNI 24

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LIGI Kuu Zanzibar inatarajiwa kufanyika tena kuanzia Juni 24, mwaka huu ili kumalizia msimu wa mwaka 2019/20 ambao ulisimama kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa corona (COVID 19 ).

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Mashindano wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Ali Mohammed Ameir, alisema ligi hiyo itachezwa katika kituo kimoja tu cha Unguja.

Ameir alisema mechi za ligi hiyo zitachezwa katika kiwanja vya Mau A na Mau na michezo itafanyika kuanzia asubuhi hadi jioni ili kukamilisha msimu kama ilivyopangwa.

Alisema siku hiyo ya kwanza kuanzia saa nane mchana Selem View yenye makazi yake Kisiwani Pemba itaumana na Maafande wa Mafunzo kwenye Uwanja wa Mau A, huku katika Uwanja wa Mau B, muda huo huo utapigwa mchezo kati ya JKU dhidi ya Mwenge.

Kuanzia saa 10:00 jioni katika Uwanja wa Mau A timu ya Zimamoto itapepetana na Mlandege, huku Mau B wakongwe wa Jamhuri watakaumana na Maafande wa Polisi.

Katibu wa JKU, Sadu Ujudi, alisema amejipanga kuhakikisha anatoka na ushindi mnono katika mchezo huo dhidi ya Mwenge na wachezaji wake wapo tayari kuendelea na mapambano ili watimize malengo yao.

Ujudi alisema nyota wa JKU wana morali, na kasi yao imerudi kivingine katika kuhakikisha lengo la kunyakua ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu linatimia.

"Tumejipanga kuhakikisha yanafanya vizuri katika mechi zetu zote, ili kutimiza malengo yetu ya msimu huu licha ya baadhi ya vilabu kuutazama kuwa ni mgumu," alisema Ujudi.

Kiongozi huyo amewataka mashabiki wa timu hiyo kuendelea kutulia kwa kufuata amri ya serikali ya kutoingia uwanjani na kufuatilia ligi hiyo kupitia matangazo ya televisheni na radio.



Deogtratius Killer (mwenye shati nyeupe), akicheza na wanenguaji wake kwenye onyesho la bendi hiyo mwishoni mwa wiki mjini Morogoro. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mwadui yaifuata Simba kwa tahadhari, umakini

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Mwadui FC kinatarajia kuwasili jijini Dar es Salaam leo kikitokea mkoani Shinyanga kwa ajili ya kuwakabili Simba katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam imeelezwa.

Mwadui ndio ilikuwa timu ya kwanza kuifunga Simba msimu huu, walipokutana katika mchezo wa mzunguko wa kwanza uliochezwa Oktoba mwaka jana kwenye Uwanja wa CCM, Kambarage.

Adam alisema kila mchezaji yuko tayari kwa mchezo huo na wanaamini wataendelea kupata matokeo mazuri dhidi ya Simba iliyoko kwenye mbio za kutetea ubingwa wanaoushikilia.

"Baada ya mchezo wa Yanga niliwapa wachezaji wangu mapumziko ya siku moja ili kuipumzisha miili, lakini kuanzia jana (juzi), tuliendelea na mazoezi kama kawaida, kwa sababu malengo yetu ni kumaliza katika nafasi za juu," alisema Adam.

Kocha hiyo aliongeza anaendelea kuzungumza na wachezaji wake ili waongeze umakini na kutorudia makosa waliyofanya katika mechi iliyopita dhidi ya Yanga ambayo walikubali kichapo cha bao 1-0.

"Sitarajii makosa yale yatajirudia tena tutakapokutana na Simba, tunatakiwa kuwa makini na kucheza kwa tahadhari kwa sababu nia na malengo yetu ni tushika nafasi nzuri katika msimamo wa Ligi Kuu Bara," Adam alisema.

Aliahidi kuibuka na ushindi katika mchezo huo ambao utakuwa na ushindani kutokana na Simba kutokubali kufungwa tena kirahisi.

Alisema wachezaji wake wameshakuwa na uzoefu na ligi hiyo tofauti na walivyokuwa katika mzunguko wa kwanza na sasa wanahitaji kusaka pointi.

"Narudia kusema, tutaingia uwanjani kwa tahadhari kwa kutambua tunajiandaa kukutana na watu ambao mpaka sasa wanaongoza katika ligi msimu huu, hatutaki kupoteza mchezo huo, tunawaheshimu na tunajua pia malengo yao," aliongeza kocha huyo.

Aliwataka wachezaji na mashabiki wao kusahau matokeo na mchezo uliopita na kufikiria kufanya vema kwenye mechi zilizobakia za ligi hiyo ya juu Tanzania Bara.

## Morogoro kamili michuano ya RCL

**Na Frank Kaundula, MOROGORO.**

JUMLA ya timu saba zinatarajiwa kushiriki katika mashindano ya mabingwa wa mikoa (RCL), yatakayofanyika kuanzia Juni 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Gairo, imefahamika.

Meneja wa Uwanja wa CCM Shabiby, Hamisi Mkailo, alisema maandalizi ya mashindano hayo yamekamilika na timu zinazotarajiwa kushiriki katika kituo hicho zitaanza kuwasili kuanzia Juni 23, mwaka huu. Mkailo alisema kuwa serikali ilifanya ukaguzi katika uwanja huo na kutoa baraka za kutumika kwenye michuano hiyo baada ya kutimiza taratibu zake.

"Kulikuwa na changamoto za hapa na pale lakini tumejitahidi kuzirekebisha kwa ajili ya michuano hii ya mabingwa wa mikoa itakayoanza kurindima kuanzia Juni 25, mwaka huu, wananchi wajiandae tena kupata burudani," alisema Mkailo.

Alizitaja timu zitakazotumia kituo hicho cha Morogoro ni pamoja na Pwani, Singida, Shinyanga, Dodoma, Arusha, Iringa na Morogoro.

"Uongozi wa kiwanja utahakikisha kuwa timu zote zinakuwa na tahadhari ya maambukizi ya virusi vya corona, na pia watu wote watakaokuwa wakiingia uwajani kutazama mechi nao ni lazima wawe na tahadhari hiyo," alisema Mkailo.

Naye Katibu wa Chama cha Soka Mkoa wa Morogoro (MRFA), Khamisi Semka, ameutaka uongozi wa uwanja huo kufuata mwongozo uliotolewa na serikali na kuzikaribisha timu zote zitakazotumia kituo hicho.

## Waluguru Original wana Morogoro Yetu

**Na Sabato Kasika**

BENDI ya muziki wa dansi ya Waluguru Original yenye maskani yake mjini Morogoro, imekamilisha nyimbo sita, ikiwa ni maandalizi ya albamu mpya kwa mwaka huu wa 2020.

Mkurugenzi wa bendi hiyo, Deogratius David 'Killer' alizitaja nyimbo hizo kuwa ni 'Morogoro Yetu, Mwanzo wa Mapenzi, Cha Kupewa, Ngalile Mwanangu Ndole, Supu na Nataka Nilewe.'

Killer alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na gazeti hili na kufafanua kuwa Waliguru Original iliandaa nyimbo hizo kabla ya shughuli za burudani kusimamishwa ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona. "Baada ya maambukizi ya corona kupungua, tumeanza maonyesho na pia tunajiandaa kwa ajili ya kurekodi nyimbo zetu ikiwa ni maandalizi ya albamu mpya kwa mwaka huu wa 2020," alisema Killer.

Mwanamuziki huyo alisema, mbali na hayo wanaendelea kuimarisha bendi yao ambayo amedai kuwa imekuwa tishio kwa bendi nyingine za muziki wa dansi mjini Morogoro na maeneo mengine ya Tanzania.

Alisema, sasa ni wakati wao wa kuendelea kujiimarisha zaidi kwa ajili ya kuwapa burudani safi mashabiki wao ambao waliikosa kwa muda mrefu mara maonyesho yaliposimamishwa.

Michezo
Jumatano Juni 17, 2020
Nipashe



Arteta: Najiamini Aubameyang atabaki Arsenal HABARI UK 22



Makocha wa Klabu ya Yanga Luc Eymael (kulia) na Boniface Mkwassa (kushoto), wakiwaangalia wachezaji Mapinduzi Balama na Haruna Niyonzima wakiwa kwenye mazoezi katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana, jioni, ikiwa ni maandalizi ya mechi yao na timu ya JKT Tanzania itakayochezwa leo uwanjani hapo. **PICHA:JOSEPH IBRAHIM**

# YANGA YATAMBA KUIADHIBU JKT

## Kocha Mbelgiji kuendelea kuwapa shangwe mashabiki wa timu hiyo, huku akijiimarisha kuelekea...

**Na Somoe Ng'itu, DODOMA**

SHANGWE zitaendelea, hayo ni maneno ya Yanga kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu Bara dhidi ya wenyeji 'Maafande' wa JKT Tanzania utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini hapa.

Hata hivyo Yanga itaendelea kumkosa mshambuliaji wake nyota Mghana Bernard Morrison ambaye alibaki jijini Dar es Salaam, akikacha kuungana na timu ilipokuwa inasafiri kuelekea mkoani Shinyanga na nahodha, Papy Tshishimbi ambaye ni majeruhi.

Akizungumza na Nipashe jijini hapa, Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, alisema kikosi chake kimejiandaa vema kuelekea mchezo huo na anaamini kila mchezaji yuko tayari kupambana kupata matokeo mazuri. Eymael alisema wachezaji wanajiandaa pia kukabiliana na ushindani kutoka kwa wenyeji wao ambao pia wanahitaji kupata pointi tatu zitakazowasaidia kukaa kwenye nafasi bora katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema wanahitaji kuongeza umaskini na kucheza kwa tahadhari kwa sababu pia wanahitaji kushinda mechi yao unaofuata ambayo itakuwa nguvu zaidi.

"Tunahitaji matokeo mazuri, tunajua tuna wakati mgumu lakini hatuna jinsi, tunatakiwa kuongeza nguvu katika kila mechi tunayocheza, mechi zote ni ngumu, pia tunatakiwa kuliweka tayari na michezo unaofuata," alisema Eymael.

Kiungo wa kimataifa wa timu hiyo, Haruna Niyonzima aliliambia gazeti hili wachezaji wote walioko jijini hapa wanausubiri kwa hamu mchezo wa leo na wakiwa na lengo moja la kuondoka na ushindi.

"Tumejipanga kusaka ushindi, tunamwomba Mungu atusaidie pia, tuko tayari kwa kila changamoto, kikubwa ni kusaka ushindi sasa na mwisho wa msimu utaamua," Niyonzima alisema.

Naye Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Mohammed Abdallah 'Bares', alisema kikosi chake kimejipanga kuisimamisha Yanga kwa sababu wanaifahamu vema timu hiyo.

"Kama wanafanya tulivyoelekezana, nina hakika pointi tatu tutazichukua, tunahitaji utulivu na kutumia nafasi tutakazopata, hata kama ni moja, na wao pia kuzika njia zao," Bares alisema.

Aliongeza wanaiheshimu Yanga kwa sababu inaondoa na wachezaji wazoefu, lakini katika mpira hakuna kukata tamaa na dakika 90 za mchezo wao zitaamua.

Yanga yenye pointi 54 iko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo, wakati JKT Tanzania ina pointi 42 na iko kwenye nafasi ya nane huku Simba ikiendelea kuwa kileleni na pointi zake 72.

Mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara raundi ya 30, inatarajiwa kuendelea tena Jumamosi kwa michezo mbalimbali, ambapo mabingwa watetezi, Simba kuwakaribisha Mwadui FC huku Jumapili Yanga ikivaana na Azam FC.

## JPM awapongeza Stars, wasanii

**Na Adam Fungamwango**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, ameipongeza timu ya taifa, Taifa Stars, pamoja na wanamichezo wote, wakiwamo wasanii waliofanya vema kwenye kipindi cha miaka mitano iliyopita, wakati yeye akiliongoza taifa.

Katika hotuba yake ya kuvunja Bunge la Tanzania, Rais ameitaja Sekta ya Michezo, Sanaa na Utamaduni ni moja kati ya sekta zinazokua kwa kasi ingawa hazisemwi sana.

Dk. Magufuli alisema kwa mujibu wa taarifa za hali ya uchumi ya mwaka 2018, shughuli za sanaa na burudani ziliongoza kwa ukuaji mwaka 2018, ambapo ilikuwa kwa asilimia 13.7 na kwa mwaka uliofuata 2019, ilishika nafasi ya tatu kwa ukuaji, ilipokuwa kwa asilimia 11.2.

Stars ilifuzu AFCON mwaka jana, chini ya uongozi wa Awamu ya Tano, Dk. Magufuli, baada ya kushika nafasi ya pili kwenye kundi L, ikimaliza kwa pointi nane, kundi lililoongozwa na Uganda iliyokuwa na pointi 13 na zote mbili zikaelekea nchini Misri kwenye fainali hizo.

## Chama akiongeza mzuka Simba

**Na Faustine Feliciane**

KUELEKEA kwenye mchezo wao wa Jumamosi dhidi ya Mwadui FC, benchi la ufundi na wachezaji wa Simba wametilia mkazo umuhimu wa mahitaji ya ushindi kwenye mchezo huo.

Kocha wa Simba, Sven Vandernbroeck, aliiambia Nipashe kuwa wachezaji wameonyesha kusikitishwa na sare waliyoipata kwenye mchezo uliopita na sasa wamepania ushindi kwenye mchezo huo huku akiweka wazi kuwa kurejea kwa kiungo wake Clatous Chama kumeongeza hali ya mapambano 'mzuka' kwenye kikosi chake.

Chama juzi na jana aliunganishwa kwenye kikosi cha timu hiyo kwenye mazoezi yake kuelekea kwenye mchezo huo wa Jumamosi na alikuwa kwenye sehemu ya timu iliyocheza mechi ya kirafiki dhidi ya Trans Camp na kuibuka na ushindi wa mabao 4-1.

Tangu kurejea nchini kutoka kwao Zambia, Chama alikuwa akifanya mazoezi kufuatana na programu alizopewa na kocha wa viungo na juzi alianza kujumuika na wachezaji wenzake kwenye mazoezi ya pamoja.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >